




## Adaiwa kumuua baba baada ya kumfuma na mke

UKURASA 3







# Nipashe

Alhamisi Aprili 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580929

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Watumiaji dawa nguvu za kiume holela hatarini

• TMDA yasema zinaua, zinaongoza kuuzwa madukani ... *Endelea Ukurasa. 2*

## YALIYOMO

UKURASA 2

### 'NYERERE HAKUKATAA DAMU YA MZUNGU'

KATIKA gazeti letu la Jumatatu Aprili 25, 2022, tuliandika habari yenye kichwa cha maneno 'Mwalimu Nyerere alikataa kuwekewa damu ya mzungu'.

UKURASA 3

### ADAIWA KUMCHOMA MTOTO KISA TAMBI

JESHI la Polisi mkoani Simiyu, linamshikilia mkazi wa Kidinda wilayani Bariadi, Mwamba Thomas (37) kwa tuhuma za kumchoma na maji ya moto mwanawe wa kiume mwenye umri wa miaka minne.



Askari wa Bunge wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Rukwa, Irene Ndyamkama, ulipofikishwa bungeni jijini Dodoma jana kuagwa na Wabunge. **Habari Uk. 7**. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

## Jafo: Kero Muungano kutatuliwa kwa vikao

UKURASA 3



## Madudu ripoti CAG yamwibua Kinana

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YAONYESHA RAMANI YA USHINDI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, akionyesha mashine ya kielektroniki ya ukusanyaji wa maduhuli ya serikali yatokanayo na makosa ya usalama barabarani, baada ya kuizindua jijini Dodoma jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Christopher Kadio, wapili ni Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Simon Sirro. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# TMDA yaonya matumizi ya dawa nguvu za kiume

**Na Sanula Athanas,** MBEYA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeonya kuwa watumiaji wa dawa za kuongeza nguvu za kiume pasi na maelekezo ya wataalamu wa afya, wako hatarini kupoteza maisha kutokana na dawa hizo kuwa na sifa ya kupanua mishipa ya damu.

Vilevile, imebanisha kuwa kwa sasa dawa hizo zinaongoza kununuliwa zaidi kwenye maduka makubwa ya dawa nchini.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Dk. Adam Fimbo, alipotoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya dawa hizo wakati wa semina kwa wahariri wa habari iliyoandaliwa na mamlaka hiyo mjini hapa jana.

Alisema kuwa ufuatiliaji wao umebaini dawa hizo kwa sasa zinaongoza kwa kununuliwa zaidi kwenye maduka makubwa ya dawa nchini, akionya kuwa zinapaswa kutumika kwa maelekezo ya daktari tu na sio vinginevyo.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema dawa hizo zinapaswa kutumiwa na mtu aliyethibitika kitaalamu kutojimudu kwenye tendo la ndoa, lakini matumizi yake, kikiwamo kiwango cha dozi, lazima yaidhinishwe na daktari.

"Watu wanakufa kwenye nyumba za kulala wageni kutokana na matumizi holela ya dawa hizi. Ufutiliaji wetu kwenye maduka ya dawa umeonyesha dawa hizi sasa zinaongoza kwa kununuliwa zaidi nchini. Zitumike kwa ushauri wa daktari tu," alisisitiza.

**USULI NA MADHARA**

Akizungumzia historia ya matumizi ya dawa hizo, Dk. Fimbo alisema: "Kuna dawa kwa ajili ya wagonjwa wa presha zilionekana kwamba moja ya 'side effects' (madhara) yake ni kuongeza nguvu za kiume.

"Kwa hiyo, baadhi ya wazalishaji wa dawa walitumia nafasi hiyo kutengeneza za dawa hizo za kuongeza nguvu za kiume. Shida ya hizi dawa ni kwamba zinasababisha kupanuka kwa mishipa ya damu. Mishipa ya damu iliyoko kichwani ikipanuka, mtu anakufa."

**UFAFANUZI KITAALAMU**

Awali, akiwasilisha mada kuhusu udhibiti wa bidhaa za tumbaku,

Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti wa Dawa, Dk. Yonah Mwalwisi, alisema dawa zinazotumika kutibu tatizo hilo zipo kwenye kundi linaloitwa phosphodiesterase type 5 (PDE5) inhibitors ambazo husababisha mzunguko wa damu kuwa mzuri ndani ya mishipa ya uume.

"Mifano ya dawa hizi ni; Sildenafil, Tadalafil, Vardenafil and Avanafil; na kati ya dawa hizi nne, tatu zimesajiliwa na TMDA na zina majina tofauti tofauti; mfano SILDENAFIL (EVOKE, ERECTO, ZWAGRA, SILMET, NJOI na VIAGRA), TADALAFIL (SAHEAL AND CIALIS) na VARDENAFIL (LEVITRA)," alisema.

Dk. Mwalwisi alisisitiza kuwa matumizi ya dawa hizo yanapaswa kufanywa na watu waliothibitika kuwa na tatizo hilo na lazima yaidhinishwe na daktari na siyo vinginevyo.

Akifafanua zaidi kuhusu angalizo lake hilo, Kaimu Mkurugenzo huyo alisema dawa hizo zinapaswa kutolewa kulingana na vigezo mbalimbali vinavyozingatiwa kitabibu, akibainisha kuwa zipo dawa za Mg 25, Mg 50 na hata Mg 100.

# Waliofanya uhalifu Chanika wadaiwa waliwahi kutumikia vifungo gerezani

**Na Romana Mallya**

KUNDI la watoto lililodaiwa kufanya uporaji na kujeruhi watu 23 usiku wa kuamkia Jumapili maeneo ya Chanika na Zingiziwa jijini Dar es Salaam, miongoni mwao waliwahi kufungwa gerezani, imeelezwa.

Hayo yalibainishwa juzi na viongozi na wananchi wa kata hizo baada ya Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, kwenda maeneo hayo na kufanya kikao maalum kujadili masuala ya kiusalama.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nguvu Mpya, Barnaba Mtumbuka, alisema vijana hao walitekeleza tukio hilo wakiwa na silaha za jadi ambazo ni mapanga, visu, rungu na nondo.

Alisema wakati wanaendesha uvamizi huo inaonyesha wengi wao ni wenyeji kwa sababu walikuwa wanawatambua kwa majina baadhi ya wananchi waliowaingilia kwenye nyumba zao.

Mwenyekiti wa wenyeviti wa kata ya Chanika, Seif Mwera, alisema baada ya tukio hilo wananchi wameelimika na kujua umuhimu wa ulinzi shirikishi.

"Wizi huu umefanywa na vijana waliopewa msamaha ambao wamekaa gerezani. Walipotoka wamerudi kwa mama zao wameona hawana cha kufanya na wamejiunga na baadhi ya wenyeji wakawapitisha na wengine. Wengine si wenyeji Kata ya Chanika," alisema.

Kamanda Muliro alisema mtu ambaye anamjeruhi mtu maana yake anataka kumpotezea maisha.

"Huyu si mtu wa huruma kupambana naye inabidi usiwe na huduma kwa mujibu wa sharia. Wazazi mnanielewa, ndugu jamaa na marafiki mnanielewa, si mimi ni sheria," alisema.

Alisema kitendo walichokifanya wahalifu hao ambao baadhi yake wanashikiliwa na upepelezi unakwenda vizuri, kila aliyeshiriki atapambana na mkono wa sheria.

"Atapambana na mkono wa chuma wa serikali, nikisema mkono wa chuma kwa mujibu wa sheria nadhani mnanielewa hatuna mzaha na suala la uhalifu, hatuna huruma na jambazi, tunamshughulikia kwa mujibu wa sheria.

"Kila mtu ana haki ya kuishi na kufanya kazi, lakini kazi halali siyo kazi za kihalifu, Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam hatukubaliana na hali hii na hatutaruhusu, ninawaonya, kama alivyosema mmoja hapa, kazi, usimamizi na malezi ya hawa vijana ukiamua kuingia kwenye kazi hii umeingia kwenye hatari."

# 'Mwalimu Nyerere hakukataa kuwekewa damu ya mzungu'

KATIKA gazeti letu la Jumatatu Aprili 25, 2022, tuliandika habari yenye kichwa cha maneno 'Mwalimu Nyerere alikataa kuwekewa damu ya mzungu'.

Habari hiyo ilikuwa ikimnukuu aliyekuwa Katibu Muhtasi wake, Anna Mwansasu katika kumbukizi ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa hayati Nyerere.

Hata hivyo, kichwa hicho cha habari kimemfadhaisha Mwansasu, licha ya maudhui kuwa sahihi kwa kuwa alikuwa akiongea kwa utani.

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza.

**Mhariri**

# Madudu ripoti ya CAG yamwibua Kinana

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, ameishauri serikali kuchukua hatua dhidi ya watumishi wa serikali waliotajwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Akizungumza jana kwenye mkutano wa ndani wa chama hicho mjini hapa, Kinana alisema wakati umefika kwa serikali kuchukua hatua kwa wahusika waliyotajwa.

"Ripoti ile inaonyesha mambo ya ovyo. Si uzushi imefanywa kisayansi na kitaaluma imeandikwa. Wabunge wameijadili kwa ukali sana. Nadhani ingekuwa vyema hatua ziwe zinachukuliwa papo kwa papo ili watu waogope kutumia vibaya fedha za umma," alisema.

Kinana ambaye alikuwa anahitimisha ziara yake ya mikoa minne kukagua uhai wa chama, alisema pamoja na kwamba hana mamlaka ya kutoa amri kwa serikali, atamwambia Rais Samia Suluhu Hassan juu ya ushauri huo.

"Kwa nafasi yangu nazungumza kwa niaba ya mwenyekiti wetu ambaye ni Rais kwamba wahusika wachukuliwe hatua," alisema na kusisitiza kuwa lazima kuwe na utaratibu wa kuwajibika mtu anapofanya kosa.

"Tujenge utamaduni wa kuwahi mtu akae pembeni apishe wengine. Si kuna wengi wana uwezo hawana kazi? Wakae pembeni waje wengine.

" Kila ripoti ya CAG inapotolewa tukianzia na hii wale wanaotajwa wajipime. Vyombo vya serikali vichukue hatua kwa yale yaliyotajwa mle (ndani ya ripoti ya CAG) ili fedha za wananchi zisichezewe," alisisitiza.

Kinana akiambata na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alihitimisha ziara yake ya mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Arusha kukagua uhai wa chama.

**ALONGA MARIDHIANO**

Katika hatua nyingine, Kinana aliwataka viongozi na wanachama wa CCM kuwa tayari kwa maridhiano ya kisiasa aliyoyaanzisha Rais Samia.

Akiwahutubia wanachama wa CCM kwenye ukumbi wa hoteli ya Mount Meru, Kinana alisema Rais ameanzisha maridhiano kati ya CCM na vyama vyote vya siasa kwa hiyo ni muhimu aungwe mkono.

"Nawaomba wana CCM wenzangu kuwa tayari kufanya maridhiano na vyama vya vya upinzani. Na wao pia nawaomba wawe tayari kufanya maridhiano na CCM na pamoja na serikali," alisema.

Kinana alisema Rais Samia ameonyesha mfano wa mzuri na wa kuigwa kwa kuanzisha mchakato huo na amekutana na vyama na taasisi mbalimbali za kisiasa.

"Juzi hapa akiwa Marekani kwenye ziara, alitaja mambo manne ambayo anayashughulikia ambayo ni mariadhiano, kuvumiliana, mabadiliko kwenye taasisi na kulijenga upya taifa," alisema na kuongeza kuwa Tanzania ni nchi ya vyama vingi vya siasa, hivyo kuwapo kwa maridhiano ni jambo muhimu sana.

"Bila maridhiano ni vigumu kupata maendeleo.. kwenye ugomvi hakuna maendeleo," alisisitiza.

# Jafo: Kero za Muungano kutatuliwa kwa vikao

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amesema ofisi yake itaendelea kuratibu utatuzi za changamoto zilizobaki na zitakazijitokeza katika utekelezaji wa masuala ya Muungano kupitia vikao.

Amesema vikao hivyo vitahusisha kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), vikiwahusisha mawaziri na makatibu wakuu.

Dk. Jafo aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/23, huku akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 53.11 kwa ajili ya matumizi ya shughuli mbalimbali.

Alisema pia kutakuwa na vikao vya kamati ndogo za fedha, uchumi na biashara na Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala vitakavyofanyika kulingana na mahitaji.

Vikao hivyo, alisema vitaratibiwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, changamoto za muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kuendelea kuuenzi, kuulinda na kuudumisha muungano wetu.

"Hivyo, wananchi waendelee kuwa na imani na serikali za pande mbili za muungano kwamba changamoto zilizobakia na ambazo kimsingi ziko katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi zitakamilishwa" alisema.

Alisema kwa mwaka 2022/23, ofisi yake itaendelea na uratibu wa masuala yasiyo ya muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya wizara, idara na taasisi za SJMT na SMZ zisizo za muungano zenye majukumu yanayoshabihiana.

Jafo alisema kwa mwaka 2022/23, pia ofisi yake itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa umma kwa makundi tofauti ya kijamii kupitia njia mabalimbali ikiwamo kupitia redio, runinga, magazeti, jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano.

"Kwa mwaka 2022/23, ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 4(3)," alisisitiza.

Aidha, Jafo alisema Ofisi ya Makamu wa Rais inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo kuendelea kuwapo kwa hoja za Muungano ambazo hazijapatiwa ufumbuzi.

Changamoto nyingine ni kutotekelezwa kikamilifu kwa mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa mazingira katika ngazi ya sekta na mamlaka za serikali za mitaa, pamoja idadi kubwa ya Watanzania kutoufahamu historia ya Muungano.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hizi, ofisi yake imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuandaa andiko la historia ya muungano litakalotumika kuelimisha umma kuhusu faida za muungano kiuchumi, kijamii na kisiasa.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tigo, CPA Innocent Rwetabura (kushoto), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, CPA Hosea Kashimba baada ya kutiliana saini mkataba kati ya MIC Tanzania PLC na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), jijini Dar es Salaam jana, kwa nia ya kupanua wigo na kuharakisha utoaji wa huduma ambapo sasa Tigo watahama Jengo la Derm Complex kwenda ofisi kubwa jengo la PSSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Atuhumiwa kumchoma mtoto kisa tambi

**Na Happy Severine,** BARIADI

JESHI la Polisi mkoani Simiyu, linamshikilia mkazi wa Kidinda wilayani Bariadi, Mwamba Thomas (37) kwa tuhuma za kumchoma na maji ya moto mwanawe wa kiume mwenye umri wa miaka minne.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Kamishna msaidizi (ACP) Shedrack Masija, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 22, mwaka huu, katika kijiji cha Kidinda.

Alisema mtuhumiwa alimchoma mwanawe kwa maji ya moto kwa madai kwamba aliiba tambi ambazo ziliandaliwa kwa ajili ya chakula cha mchana.

Masija alisema mtuhumiwa alimchoma mwanawe mikononi na sehemu mbalimbali za mwili baada ya kugundua kuwa alikula tambi hizo, hivyo kumsababishia majeraha sehemu za mwili wake.

Kamanda Masija alisema mtoto huyo amelazwa Hospitali ya Wilaya ya Bariadi kwa ajili ya matibabu na kwamba afya yake inaendelea kuimarika

Alisema jeshi hilo linaendelea kumshikilia mtuhumiwa huyo mpaka uchunguzi utakapokamilika na kisha jalada lake litafikishwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wilaya ya Bariadi ya Somanda, Dk. Emmanuel Constantine, alithibitisha kupokea mtoto huyo na kusema amelazwa wodi ya 3D (ya watoto) na anaendelea vizuri.

# Adaiwa kumuua babaye baada ya kumkuta amelala na mkewe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia Mwandu Shija (32) mkazi wa Ndala Manispaa ya Shinyanga, kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi, Shija Robert (55), kwa madai ya kumfumania akiwa amelala na mke wake kitandani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira saa 8:00 usiku.

Kyando alisema kijana huyo aliporudi nyumbani, alimkuta baba yake akiwa amelala na mke wake na kuanza kumshambulia.

Alisema wakati kijana huyo akiendelea kumshambulia baba yake na kipande cha kuni sehemu mbalimbali za mwili wake, ndipo alipompiga sehemu mbaya na kusababisha mauaji. "Chanzo cha tukio hili ni wivu wa kimapenzi., baada ya marehemu kukutwa akiwa amelala kitanda kimoja na mke wa mtuhumiwa," alisema Kyando.

"Mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi na daktari na kuhifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa mkoani Shinyanga, ukisubiri kukabidhiwa kwa wanandugu kwa ajili ya maziko," aliongeza.

Kamanda Kyando pia alisema Jeshi la Polisi mkoani hapa linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

# TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|---|
| | | | 31.03.2022 | 31.12.2021 |
| A. | | MALI | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 47,576 | 49,972 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 46,526 | 16,534 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 104,766 | 133,175 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 69,805 | 73,818 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 423 | 284 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 139,037 | 124,636 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 732,994 | 718,600 |
| | 12 | Mali Nyingine | 49,040 | 44,907 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 21,412 | 22,599 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,211,580** | **1,184,525** |
| B | | DHIMA | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 768,387 | 729,137 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 169,724 | 178,978 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 4,997 | 3,988 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | (0) | (0) |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 19,420 | 17,858 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 2,365 | 2,429 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 28,169 | 28,383 |
| | 28 | Madeni | 103,672 | 108,575 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,096,734** | **1,069,349** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **114,845** | **115,176** |
| C. | | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 75,200 | 65,433 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,880 | 11,238 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 10,433 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **114,845** | **115,176** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 195,905 | 208,231 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 81,111 | 80,859 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 14,848 | 15,554 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 11 | 11 |
| D. | | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.48% | 9.72% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 10.77% | 10.94% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80.27% | 101.34% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.50% | 60.67% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80.62% | 80.66% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 3.30% | -3.48% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 2.28% | 4.43% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 31-Mar-22 | 31-Mar-21 | 31-Mar-22 | 31-Mar-21 |
| 1 Mapato ya Riba | 34,722 | 32,058 | 34,722 | 32,058 |
| 2 Gharama za Riba | (10,604) | (9,529) | (10,604) | (9,529) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **24,119** | **22,529** | **24,119** | **22,529** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (16) | (1,619) | (16) | (1,619) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,481) | (3,548) | (3,481) | (3,548) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **7,904** | **8,890** | **7,904** | **8,890** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 1,422 | 1,159 | 1,422 | 1,159 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,139 | 4,563 | 4,139 | 4,563 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 2,342 | 3,168 | 2,342 | 3,168 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(24,673)** | **(21,737)** | **(24,673)** | **(21,737)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 12,346 | 11,242 | 12,346 | 11,242 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1,554 | 1,187 | 1,554 | 1,187 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 10,773 | 9,308 | 10,773 | 9,308 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,853** | **4,516** | **3,853** | **4,516** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,973 | 1,950 | 1,973 | 1,950 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,880** | **2,566** | **1,880** | **2,566** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,880** | **2,566** | **1,880** | **2,566** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,089 | 1,068 | 1,089 | 1,068 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 67 | 91 | 67 | 91 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 47 | 43 | 47 | 43 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.16% | 0.25% | 0.16% | 0.25% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.63% | 2.41% | 1.63% | 2.41% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 57.88% | 53.08% | 57.88% | 53.08% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.46% | 2.74% | 2.46% | 2.74% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31-Mar-22 | 31-Dec-21 | 31-Mar-22 | 31-Mar-21 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 3.853 | 4.786 | 3.853 | 4.516 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 5.939 | 8.083 | 5.939 | 7.450 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (14.394) | (36.612) | (14.394) | (36.911) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 29.996 | (3.392) | 29.996 | (24.437) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2.611) | 1.687 | (2.611) | (1.267) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (4.133) | 1.724 | (4.133) | (3.425) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (1.973) | (1.950) | (1.973) | (1.950) |
| | - Menginevo (bainisha) | 19.362 | 7.020 | 19.362 | (9.947) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **36,040** | **(18,654)** | **36,040** | **(65,972)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (980) | (3.725) | (980) | (1.591) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa | - | - | - | - |
| | Menginevo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(980)** | **(3,725)** | **(980)** | **(1,591)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (1,798) | (1,122) | (1,798) | (1,513) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(1,798)*** | ***(1,122)*** | ***(1,798)*** | ***(1,513)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 33,261 | (23,501) | 33,261 | (69,075) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **111,676** | **135,177** | **111,676** | **120,526** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 144,937 | 111,676 | 144,937 | 51,451 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI, 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | **(248)** | - | - | | **(248)** |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 1,880 | **1,880** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **75,200** | **(0)** | **0** | **11,574** | **114,845** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 9,167 | - | - | - | **9,167** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (253) | - | - | - | **(253)** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI, 2022

Benki ililipa faini ya shilingi 1,000,000 kwa kuchelewa kuwasilisha taarifa ya kila siku(NOP)

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe
kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | **Imesainiwa** | **27.04.2022** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | **Imesainiwa** | **27.04.2022** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | **Imesainiwa** | **27.04.2022** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

DR. EDMUND B. MNDOLWA
**Mwenyekiti wa Bodi** **Imesainiwa** **27.04.2022**

MS. ANNE C. MBUGHUNI
**Mjumbe wa Bodi** **Imesainiwa** **27.04.2022**

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

## TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | MINIMUM OPERATING BALANCE | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | 7,000.00 | 5.00 | 50,000.00 | 100.00 |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | FREE | N/A | 50,000.00 | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | 1,560.00 | 0.86 | 20,000.00 | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | 1,560.00 | N/A | 0 | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000.00 | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | FREE | FREE | 50,000.00 | N/A |
| Platinum Account | 15,000.00 | N/A | 1,560.00 | N/A | 15,000 | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | FREE | N/A | 20,000 | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 6 | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000 | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | FREE | N/A | 30,000 | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | 1,560.00 | N/A | 10,000 | N/A |
| Wadu Account | 20,000.00 | N/A | FREE | FREE | 20,000 | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | 700.00 | N/A | 1,500.00 | N/A |

| CASH SERVICES | | |
|---|---|---|
| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
| Cash deposit | | FREE |
| | Withdrawal below 400,000 | 1,800.00 |
| | Withdrawal 400,001 - 800,000 | 3,000.00 |
| | Withdrawal from 800,001 - 1,200,000 | 4,400.00 |
| | Withdrawal from 1,200,001 - 10,000,000 | 5,000.00 |
| | Withdrawal from 10,000,001 - 50,000,000 | 6,000.00 |
| | Withdrawal from 50,000,001 -100,000,000 | 14,000.00 |
| Cash withdrawal TZS | Withdrawal from above 100,000,000 | 30,000.00 |
| | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| BANK STATEMENT | TZS | USD |
| Balance enquiry over the counter | 300.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| CHEQUE SERVICE | TZS | USD |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

| DORMANT ACCOUNT | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

| GUARANTEE | |
|---|---|
| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

| AGENT BANKING SERVICE | | |
|---|---|---|
| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 3,000, 000.00 | 10,000.00 |
| Balance Enquiry | | 100.00 |
| Mini Bank Statement | | 200.00 |

| POPOTE ATM SERVICE | |
|---|---|
| DESCRIPTION | CHARGES |
| Popote ATM card Issuance/Replacement | 5,000.00 |
| PIN Re-issue | FREE |
| Collection of ATM Card at non-Domicile Branch | 6,500.00 |
| Uncollected and Destroyed ATM Card | 6,500.00 |
| Balance Enquiry | 300.00 |
| TCB ATM Withdrawal | 1,300.00 |
| Withdrawal to Other Bank Umoja Switch ATMs | 1,300.00 |

| POPOTE VISA CARD | |
|---|---|
| DESCRIPTION | CHARGES |
| Popote VISA issuance/Replacement | 20,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,350.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 5,500.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |

| POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING | | |
|---|---|---|
| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
| Registration | | FREE |
| | 500 -10,000.00 | 850.00 |
| | 10,000.01 - 50,000.00 | 1,200.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 1,500.00 |
| | 100,000.01 - 250,000.00 | 2,800.00 |
| | 250,000.01 - 500,000.00 | 4,600.00 |
| | 500,000.01 - 750,000.00 | 7,500.00 |
| Transfer Bank to MNO | 750,000.01 - 1,000,000.00 | 10,000.00 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

| LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES | | |
|---|---|---|
| LOANS | CATEGORY | INTEREST RATE |
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 10,000.00 |
| | Loan Application fee | TZS 10,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 10,000.00 Maximum TZS 100,000.00 |
| | MIC loan Application fee | TZS 25,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 50,000.00 |
| | Loan Applicationfee for Business and Personal Loans | TZS 50,000.00 |
| Interest Rates and Charges On Business Loan | Loan Administration fee- Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |




Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683
Namba bila Malipo: 0800110160

216827701

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TEHAMA muhimu Kikosi Kazi kupata maoni mengi

NI habari njema kuwa Kikosi Kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan, kinachofanyia kazi masuala ya demokrasia ya vyama vingi vya siasa , kimeanza kupokea maoni na mapendekezo ya wadau.

Ofisi ya Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, amewatangazia wananchi na taasisi mbalimbali kwenda kwenye mikutano ya hadhara na ya ndani kuwasilisha maoni yao.

Maoni yanalenga katiba, uchaguzi, mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu, umoja wa kitaifa, ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa na demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Mengine ni elimu ya uraia, rushwa na maadili katika siasa na uchaguzi, ruzuku ya serikali kwa vyama vya siasa, uhusiano wa siasa na mawasiliano kwa umma.

Katika tangazo hilo wametaja eneo la mkutano huo kuwa ni ukumbi wa Adam Sapi wa ofisi ndogo ya Bunge mkoani Dar es Salaam na kikosi kinaanza kukutana na wadau kupokea maoni na mapendekezo yao.

Wadau wakiwamo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Jukwaa la Katiba (JUKATA) na Baraza la Habari Tanzania (MCT) ni miongoni mwa wanaotajwa.

Wengine ni pamoja na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Kanisa la Sabato Tanzania, Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na wengine wengi.Wakati kikosi kazi hiki kinakwenda kuanza jukumu hilo, Watanzania hawajasahau kazi iliyofanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Warioba, ambayo iliwafikia wananchi mbalimbali kupokea maoni yao na kuandaa rasmu ya katiba.

Andiko hilo lilifikishwa kwenye Bunge la Katiba, lakini mchakato haukuwaletea katiba mpya, huku kundi moja likisusia licha ya baadaye ilipatikana Katiba Inayopendekezwa ambayo baadhi ya watu waliifananisha na kivuli cha katiba ya mwaka 1977 inayotumika leo.

Ni ushauri wetu kwa kikosi kazi kuwafikia wadau wote ili kujua kile wanachokitaka. Tukumbuke wakati wa Jaji Warioba walifanya mikutano na wananchi vijijini ambao walieleza wanataka katiba ibebe nini kwa kuwa ndiyo muongozo wa maisha ya Watanzania.

Pamoja na kukutana na baadhi za taasisi zikiwamo za kidini tunashauri kuhakikisha wananchi wengi wanafikiwa ili maoni au mapendekezo yatakayofikishwa kwa Rais Samia, yawe yamekibeba kile Watanzania wanachotaka kifanyike ili kuwa na uwanja sawa kudumisha demokrasia, kuleta maendeleo ya uchumi ya raia na taifa.

Ni ushauri wetu kwa kikosi kutengeneza mfumo wa kupokea maoni kwa mtandao ili kuwe na uwanja mpana wa watu wengi zaidi kutoa maoni yao, ili wanapokuja kuandika ripoti isheheni mawazo na maoni ya wengi. Tunaamini kuwa kwa kutumia teknolojia kazi ya kuchukua maoni itakuwa siyo ya gharama kubwa kwa vile wakati mwingine, hakutakuwa na ulazima wa kusafiri kwenda maeneo mbalimbali kwa vile itawezesha kuwafikia wananchi wengi zaidi ambao wataeleza kile wanachoona kinafaa kwa njia ya kielektroniki.


Kuwapo kwa watu wengi na maoni mengi kutaondoa hisia kuwa wajumbe walikwenda kukusanya maoni wakiwa na ripoti au majibu waliyotayarisha kabla.

Tunaamini ushirikishwaji mkubwa wa sauti za umma ipasavyo kile kitakachofikishwa kwa Rais na baadaye kufanyiwa maamuzi kitakuwa na tija kwa maisha ya kila Mtanzania.

Katka dunia ya sasa yenye ukuaji wa demokrasia watu wana hiari ya kuchagua wanachoona kinawafaa, lakini ni wakati ambao kuna vyama vingi ambavyo ni uamuzi binafsi kuwa mfuasi wa chama fulani na kwa kuwa moja ya kazi ya kikosi hicho ni kuangalia demokrasia ya vyama vingi ni muhimu wakafanya kazi yao kwa misingi ya haki na weledi na kuepuka kutaka kuwaridhisha watawala.

Tunaamini wakipata sauti sahihi na za wengi watamfikishia Rais ujumbe wenye uhalisia ili kuwezesha kufanya maamuzi, kwa kuwa ndani yake kuna mambo makubwa na magumu kama la katiba mpya, ambalo Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alilianzisha lakini halijafanikiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wazazi kuweni makini na watoto kwa Iddi ijayo

Na Adam Fungamwango

**ZIMEBAKI** siku chache sana, waumini wa dini ya Kiislam nchini Tanzania, waungane wa wenzao dunia nzima kuadhimisha Sikukuu ya Idd El Fitri, ikiwa ni maadhimisho ya kumaliza mfungo mtukufu wa Ramadhani.Kwanza, tunawapongez sana.

Nchini Tanzania kama zilivyo sikukuu nyingine, huwa na shamrashara nyingi, wananchi huadhimisha kwa njia mbalimbali.

Kuna wanaobaki tu majumbani mwao na familia zao, lakini wapo wanaoenda kutembelea ndugu na jamaa. Hapa nchini, maadhimisho ya sikukuu karibuzote hufanana.

Hata hivyo, kwa miaka ya karibuni kumezuka tabia ya baadhi ya wazazi kuwaacha watoto wao kutoka majumbani na kwenda kutembea kwa ajili ya kusherehkea sikukuu, wenyewe husema 'wanakwenda kwenye sikukuu.'

Mara nyingi watoto majirani kuanzia miaka umro miwili hadi 10, wanaocheza pamoja hujikusanya na kuondoka pamoja majumbani mwao, kwenda sehemu mbalimbali kwa ajili ya kusherehekea sikukuu.

Wakati mwingine hao wote huongozwa na mtoto wa miaka 15, ambaye yeye ndiye mlinzi wa wengine. kwa sababu akili yake inaonekana imeanza kukomaa.

Huyo anawaongoza ili wasizozane, kugombana na wakati mwingine kazi yake kubwa ni kuwavusha barabara.

Kuna wakati mpango unaanikiwa, pia wakati mwingine inafeli. Ni kwamba inategemea wanakwenda wapi na kufanya nini.

Tumeshuhudia kuna wakati watoto hao wanashawishiana kwenda kwenye muziki, ambao ni maarufu kama 'disko toto'.

Hiyo ni hatari sana, kwa sababu wakati mwingine watoto wanaenda kuingia kwenye kumbi, ambazo zimeezekwa juu.

Kumbi hizo ni maalum kwa wakubwa tu, lakini watoto wanatakiwa hata kama wanakwenda kujiburudisha kwenye 'disko toto', lakini zinatakiwa ziwe za wazi.

Sehemu zao zinatakiwa ziwe kama zile za michezo ya watoto kama kuendesha farasi, bembea na burudani zingine huwa tunaona ni za wazi, labda pembeni kunakuwa na vizuizi kama vile ukuta, ili waingie na viingilio. Kutokana na hilo disko linatakiwa liwe hata kwenye viwanja vya mpira, kwa sababu juu ni wazi.

Miaka 14 iliyopita, Oktoba 2008, watoto 19 wenye umri kati ya miaka 12 mpaka 17 walifariki mkoani Tabora kwenye ukumbi baada ya kutokea mkanyagano.

Ni 'disko toto' lililoandaliwa kwa sherehe za sikukuu kama hii, mbali na hao kufariki, wengine walijeruhiwa na kulazwa, kwa mujibu wa polisi ilitokana na kukosa hewa wakiwa ndani, hivyo baada ya kutaka kutoka nje kwa pamoja, walianza kukanyagana.

Siyo lazima mpaka makamanda wa polisi waanze kutoa tahadhari kwa wazazi. Usalama wa mtoto zaido uko kwa mzazi mwenyewe.

Wazazi wanatakiwa wawe na watoto wao, badala ya kuwaachia madada wa kazi kutembea nao, huku wao wakiwa wamekwenda kwenye starehe zao zingine.

Na wala hawawabani, kinachotakiwa ni kuwachukua mchana na kuwapeleka wenyewe sehemua ambazo wazazi wataona watoto zao watafurahi, hata kama kwenye 'disko' toto, lakini iwe sehemu salama.

Halafu ukiingia usiku wanawarudisha nyumbani na wao wanaondoka kwenye kwenye starehe za kikubwa.

Hiyo itawaepusha watoto kwenda sehemu ambazo si salama.

Kuna baadhi ya watoto kuanzia miaka 15 hadi 17, hawa nao wamekuwa na tabia za kwenda sehemu mbalimbali hatarishi.

Mfano ni kwenye jiji la Dar es Salaam, huwav wanakodisha magari ambayo hufanya vibweka barabarani, wakihatarisha usalama wao na watumiaji wengine.

Huko kwenye fukwe wanakoenda nako ni matatizo matupu. Wanafanya vitu ambavyo si tu havina maadili, pia baadhi wanajilazimisha kuogelea wakati ndiyo mara ya kwanza wanaiona bahari, hivyo wanahatarisha pia usalama wao.

Hawa watoto wakubwa kidogo wanatakiwa kuonywa, kutadharishwa na kuelezwa athari za kitakachotokea watapotoroka majumbani na kwenda huko.

# Irene alivyoagwa kwa vilio, simanzi bungeni

**Na Gwamaka Alipipi**, DODOMA

SIMANZI, majonzi jana vilitawala katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma wakati wa kuaga mwili wa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Irene Ndyamkama, aliyefariki dunia Jumapili katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha mkoani Pwani.

Shughuli ya kuaga kwa mwili wa Irene ziliongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wabunge na wa kidini.

Mbunge huyo alifariki dunia katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha mkoani Pwani, baada ya kuugua ghafla akiwa safarini kuelekea Dar es Salaam.

Mwili wake ulifikishwa katika viwanja vya Bunge saa 5:10 asubuhi na kufanyiwa ibada iliyoongozwa na Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Elikana Gonda. Akizungumza wakati wa ibada ya kuaga mwili, Dk. Mpango aliwataka wabunge wanawake kuiga mfano wa Irene wa kuwa mzalendo na Taifa lake.

Dk. Mpango alisema: Wabunge wanawake muige tabia nzuri ya Irene. Hata sisi viongozi tunajambo la kujifunza la uzalendo kwa Taifa. Kila mtu akaige mfano wa Irene aliokuwa nao wa kuwa mzalendo kwa Taifa, kuwajali wengine." Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema: "Enzi za uhai wake Irene alikuwa akipita kwetu (mawaziri) kutueleza changamoto za Mkoa wa Rukwa. Tuna kazi ya kumuenzi na kuendeleza yale aliyoyaacha."

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema: "Irene aliishi na watu vizuri, alieshimu kila mtu, alikuwa na upendo, heshima, alikuwa mtu wa kumsalimia kila mtu."

Mwakilishi wa wabunge wanawake (TWPG), Agness Hokololo, alisema Irene alikuwa mcheshi, mchangamfu, kwamba kifo chake kimeacha pengo. Mwakilishi kutoka Kambi ya Walio Wachache bungeni, Sophia Mwakagenda, alisema: "Tumefanya kazi na Irene kwa mwaka mmoja na nusu kabla ya kurudi CCM. Alikuwa anachipukia katika siasa. Alikuwa mbunge aliyepigania maendeleo ya eneo lake."

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile, alisema: "Siku ya Jumamosi tulikwenda Dar es Salaam kwa ndege kutembelea viwanda lakini Irene hatukuongozana naye, aliondoka na gari. Sisi tuliwahi kufika. Kesho yake tunajiandaa kurudi Dodoma tukapata taarifa kwamba Irene ametangulia mbele ya haki."

**WASIFU WA MAREHEMU**

Akisoma wasifu wa marehemu, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Zodo alisema Irene alizaliwa Oktoba 15, 1987 katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam.

Alisema mwaka 1992 hadi 1999, Irene alisoma Shule ya Msingi Bunge jijini Dar es Salaam, mwaka 2001 hadi 2005 alisoma Shule ya Sekondari Igolest nchini Uganda.

Zodo alisema mwaka 2005 Irene alihitimu masomo ya Kompyuta ngazi ya cheti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), mwaka 2006 hadi 2007 alihitimu kidato cha sita nchini Uganda.

Mwaka 2008 hadi 2011 Irene alisomea Shahada ya Utawala na Usimamizi wa Biashara nchini Marekani na mwaka 2014 hadi anafariki alikuwa mwanachama wa CCM, Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Irene anatarajiwa kuzikwa kesho mkoani Rukwa

# Wenye mabasi watishia kusitisha huduma

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) kimetishia muda siyo mrefu kama hakutakuwa na mabadiliko ya kupanda kwa nauli, abiria watashuhudia mabasi yakiegeshwa.

Katibu Mkuu wa TABOA, Joseph Priscus, alitoa kauli hiyo katika mjadala ulioendeshwa na kurushwa na Kituo cha Televisheni cha EATV uliokutanisha wadau wa usafiri kujadili kupanda kwa nauli vyombo vya moto. Pristus alisema wao wanashauri nauli zipandishwe, lakini ziwe rafiki kwa mlaji kwa maana muda siyo mrefu abiria watakosa huduma kwa sababu wamelemewa na madeni ambayo hawawezi kuyalipa.

"Madeni ya matairi hatuwezi kulipa, wasambazaji wetu wakitukatia huduma kuna basi litakuja stendi bila matairi? Kuna basi litakwenda safari bila mafuta?" alihoji na kuendelea: "Sababu kubwa za bei za nauli zipande ni mbili, moja ya muda mrefu ongezeko la gharama za mtaji bei ya gari na daladala, gari imepanda kwa zaidi ya asilimia 100, gharama za uendeshaji, matairi yamekuwa yakipanda kidogo kidogo. "Sababu ya pili ni suala la kupanda mafuta tulikuwa tukinunua kwa Sh. 1,900 hadi 2,000, petroli imefika hadi Sh/ 2,900, tunajua tunabeba watu wa kawaida, lakini hatuna namna ni vitu vilivyo juu ya uwezo wetu ili tuendelee kutoa huduma hatuna namna.' Hoja ya kupandisha nauli iliungwa mkono pia na msemaji wa Chama cha Wafanyakazi Madereva Tanzania (TADWU), Stanley Kilave, ambao nao wamelalamikia gharama za uendeshaji ni kubwa. Kilave alitoa mfano wa daladala za masafa ya mjini ambapo kwa gharama za sasa wanajikuta kuanzia asubuhi mpaka jioni wanaweka mafuta ya Sh. 160,000 na kazi inayofanyika ni ya Sh. 250,000 hivyo fedha yote inaishia barabarani kutokana na gharama wanazobeba.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa CHAKUA, Hassan Mchanjama, alisema msisitizo wao ni nauli zibaki kama zilivyo kwa sababu hata zilizopo bado hazijafikia bei elekezi.

"Muda mwingi abiria tunachajiwa chini ya hapo, watumie bei elekezi iliyopo sasa ambayo kimsingi wananchi wengi hawajui," alisema. Mchanjama alisema ni kweli mafuta yamepanda na kufafanua kuwa sekta ya usafirishaji ndiyo mama, hivyo isichukuliwe tu kwamba kwa sababu gharama nyingine zimepanda basi nauli nazo zipandishwe. Alifafanua baadhi ya watoa huduma wanalifanya suala hilo kisiasa zaidi ya uhalisia hasa kwa kuangalia hoja wanazitoa.

"Utaratibu wa usafirishaji lazima ulete ukokotoaji unaoleta ukweli kwamba mtu anapata hasara, ukiangalia kwa sasa hali halisi iliyopo sokoni hata ukienda stendi mbalimbali kama wakijibana vizuri wasingepiga kelele za gharama," alifafanua. Kaimu Mtendaji wa LATRA-CCC, Leo Ngowi, alisema baada ya kuona mafuta yamepanda na wamiliki wamewasilisha kwao hoja ya nauli zipande walifanya utafiti mdogo wa kufuatilia kimtandao mafuta yanauzwa shilingi ngapi. Alisema walijiridhisha walau wanaweza kujua bei ya mafuta inayouzwa popote nchini na pia waliangalia uhalisia wa maisha kwa kuongea na wadau na wakabaini nauli zilizopo sasa zinakidhi mahitaji.



## FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED

1st Housing

### UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.03.2022

**IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014**

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2022**

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31st Mar. 2022 | Robo Mwaka iliyopita 31st Dec. 2021 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 558 | 615 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,652,765 | 3,601,639 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,022,266 | 945,171 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 14,435,215 | 13,570,278 |
| 12 | Mali Nyingine | 746,297 | 575,929 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,622,000 | 1,622,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 405,140 | 449,612 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **23,884,242** | **20,765,244** |
| | | | |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 418,073 | 488,087 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 650,138 | 1,008,249 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 234,086 | 41,070 |
| 27 | Dhima Nyingine | 463,311 | - |
| 28 | Madeni | 3,849,858 | 1,010,685 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **5,615,465** | **2,548,091** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **18,268,777** | **18,217,153** |
| | | | |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,800,000 | 21,800,000 |
| 32 | Malipo juu ya bei ya hisa | - | - |
| 33 | Akiba ya Mtaji | 95,831 | 95,831 |
| 34 | Mapato Yaliyobakizwa | (3,710,587) | (3,935,988) |
| 35 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 51,623 | 232,962 |
| 36 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 31,909 | 24,348 |
| 37 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 38 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,268,777** | **18,217,153** |
| 39 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 40 | Mikopo Chechefu | 316,575 | 329,009 |
| 41 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 63,382 | 55,648 |
| 42 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 76.49% | 87.73% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.19% | 2.39% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 3556.18% | 2825.75% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.44% | 65.35% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 90.08% | 88.34% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -14.34% | 18.16% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 15.02% | 2.94% |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| Jina na Cheo : | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Sasa M. Chonza **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |
| Amulike Kamwela **(Mkuu wa Fedha)** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |
| Isambo Binde **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2022**

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Maelezo | Robo ya Mwaka sasa 31st Mar. 2022 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31st Mar. 2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31st Mar. 2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31st Mar. 2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 694,097 | 521,782 | 694,097 | 521,782 |
| 2 | Gharama za Riba | (69,467) | (28,556) | (69,467) | (28,556) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **624,629** | **493,227** | **624,629** | **493,227** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (7,734) | 9,571 | (7,734) | 9,571 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **85,774** | **36,227** | **85,774** | **36,227** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 38 | 26 | 38 | 26 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 53,350 | 36,198 | 53,350 | 36,198 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 32,386 | 2 | 32,386 | 2 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(647,147)** | **(525,128)** | **(647,147)** | **(525,128)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (326,130) | (233,488) | (326,130) | (233,488) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (321,017) | (291,640) | (321,017) | (291,640) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **55,523** | **13,896** | **55,523** | **13,896** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (3,899) | (2,790) | (3,899) | (2,790) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **51,623** | **11,106** | **51,623** | **11,106** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya mwaka /mwaka** | **51,623** | **11,106** | **51,623** | **11,106** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 20 | 18 | 20 | 18 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.24 | 0.05 | 0.24 | 0.05 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.23% | 0.05% | 0.23% | 0.05% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.28% | 0.06% | 0.28% | 0.06% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 91.10% | 99.18% | 91.10% | 99.18% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.13% | 2.73% | 3.13% | 2.73% |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2022**

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo ya mwaka ya sasa (31.03.2022)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya mwaka (01.01.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,703,026)** | **24,348** | **-** | **95,831** | **18,217,153** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 51,623 | - | - | - | 51,623 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (7,561) | 7,561 | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.03.2022)** | **21,800,000** | **-** | **(3,658,964)** | **31,909** | **-** | **95,831** | **18,268,777** |
| | | | | | | | |
| **Robo ya mwaka iliyopita (31.12.2021)** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka (01.10.2021)** | **21,800,000** | **-** | **(3,828,590)** | **35,191** | **-** | **95,831** | **18,102,432** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 114,721 | - | - | - | **114,721** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | **10,843** | **(10,843)** | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa robo ya mwaka (31.12.2021)** | **21,800,000** | **-** | **(3,703,026)** | **24,348** | **-** | **95,831** | **18,217,153** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi).

| Jina: | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Sanjay Suchak** Mwenyekiti | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |
| **Vinod Rustagi** Mkurugenzi | (Imesainiwa) | 25.04.2021 |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2022**

*(Kiasi kwa shilingi elfu)*

| | | Robo ya Mwaka sasa 31st Mar. 2022 | Robo ya Mwaka iliyopita 31st Dec. 2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31st Mar. 2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31st Mar. 2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **55,523** | **249,392** | **55,523** | **13,896** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 87,616 | 321,866 | 87,616 | 77,389 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (891,093) | (7,376,039) | (891,093) | (1,707,160) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (70,014) | 75,000 | (70,014) | 4,986 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 294,316 | (50,276) | 294,316 | 573,233 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (166,469) | (44,042) | (166,469) | 36,690 |
| | - Kodi iliyolipwa | (3,899) | (12,917) | (3,899) | - |
| | - Mengineyo | 52,923 | (5,640) | 52,923 | 30,347 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | ***(641,099)*** | ***(6,842,656)*** | ***(641,099)*** | ***(970,620)*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | 35,130 | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (16,988) | (48,243) | (16,988) | (418,001) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (51,126) | (1,059,492) | (51,126) | (1,115,279) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(68,113)*** | ***(1,072,605)*** | ***(68,113)*** | ***(1,533,279)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Deni jipya kutoka CRDB Bank | 2,839,173 | - | 2,839,173 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (49,702) | (95,154) | (49,702) | (49,695) |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | ***2,789,471*** | ***(95,154)*** | ***2,789,471*** | ***(49,695)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na** | **2,080,259** | **(8,010,415)** | **2,080,259** | **(2,553,594)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | 945,786 | 8,921,409 | 945,786 | 8,921,408 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo ya mabenki | (3,221) | 34,792 | (3,221) | 19,143 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **3,022,824** | **945,786** | **3,022,824** | **6,386,957** |

**MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES**

| S/No | ITEMS | CHARGES/FEES |
|---|---|---|
| 1 | Prime Lending Rate (PLR) | 18% p.a. |
| 2 | Maximum spread above PLR | 4% p.a. |
| 3 | Application Fee (Non-refundable) | TZS 200,000/- |
| 4 | Processing Fee | 1.5 % of the loan value |
| 5 | Facility Fee | 1.5 % of the loan value |
| 6 | Valuation Fee | Paid by the client as per the invoice |
| 7 | Legal Fee | Paid by the client to FHF account and FHF will pay law firm |
| 8 | Early Repayment | 5% of the amount to be prepaid |
| 9 | Annual Review Fee | NIL |
| 10 | Cheque returned Unpaid (Outward & Inward) | TZS 50,000/- |
| 11 | Loan Statement | TZS 20,000/- |



# Uzinduzi Royal Tour kufunika Arusha leo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ZAIDI ya watu 5,000 wakiwamo viongozi wa serikali Tanzania na Zanzibar, wanatarajia kushiriki uzinduzi wa filamu maarufu ya Royal Tour utakaofanyika leo kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Arusha (AICC).

Akizungumza jana jijini hapa, Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongela, aliwaomba wananchi kujitokeza leo saa 12:00 asubuhi kumpokea Rais Samia Hassan Suluhu atakayekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo.

Pia aliomba viongozi wote watakaoshiriki uzinduzi huo aliwaomba wafike saa 5:00 asubuhi Hoteli ya Mount Meru kuegesha magari yao na kupanda usafiri wa pamoja hadi AICC.

"Hapa tunaweka utaratibu huu ili wawahi ukumbini na wote wawe wamefika eneo la matukio saa nane kamili mchana kwa sababu Rais Samia akishaingia ukumbini hataruhusiwa mtu kuingia AICC,"alisema

Mongella, alisema wananchi watakaojitokeza kushuhudia uzinduzi huo AICC wameandaliwa eneo maalum la kukaa lenye uwezo wa kubeba watu zaidi ya 6000.

"Hapa nawaomba wananchi mjitokeze luka kushuhudia tukio hilo, ambalo tunaandika historia ya nchi yetu na kila mtu atapata pa kukaa bila shida, wala msiongope kuja ni tukio la kila mwananchi bila ubaguzi wa aina yoyote,"alisema.

Aliomba pia sekta binafsi kujiandaa vyema kwenye kampuni zao kwa ajili ya kupokea wageni kwani baada ya uzinduzi huo wanatarajia kupokea watalii wengi.

Mongella, alisema Rais amefungua milango na kinachotakiwa sekta binafsi kujipanga katika kuimarisha huduma zao.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha Justine Masejo, alisema Jeshi la Polisi limejiimarisha ili kuhakikisha usalama unakuwepo zaidi ya siku zote.

Filamu hiyo ilizinduliwa Aprili 18 New York ,Aprili 21 mwaka huu, Los Angeles nchini Marekani na leo mkoani Arusha, kisha Mei 7 Zanziba na Mei 8 Dar es Salaam.

Waandaaji wa Filamu hiyo, Peter Greenberg na timu yake ya Royal Tour na ilirushwa na vituo vya Televisheni 350 na wameweka kwenye Applications za Amazon Prime na Apple TV Plus ikiwa na lengo la kutangaza na kuifungua nchi kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa watalii na wawekezaji ili kukuza uchumi wa nchi.



Daktari kutoka hospitali ya wilaya ya Tarime akihudumia watoto wakati wa maadhimisho ya Siku ya Malaria yaliyofanyika katika viwanja vya Sekondari ya Igwe juzi chini ya udhamini wa Barrick North Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TANESCO yajipanga kuongeza transfoma kubwa za dharura

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, amesema wanajipanga kuwa na transfoma kubwa moja au mbili zaidi za akiba kwenye kituo kikuu Dodoma ili kusaidia kutoa msaada kwenye mikoa mingine litapotokea tatizo la kuharibika au kuungua kama ilivyotokea mkoani Morogoro.

Chande alitoa kauli hiyo jana mkoani Morogoro alipotembelea kituo cha kupokea, kupooza na kusambaza umeme cha Msamvu wakati ufungaji wa transfoma mpya yenye thamani ya Sh. bilioni 2 ukiendelea baada ya trasfoma iliyokuwapo awali kuungua mapema Aprili mwaka huu.

Alisema ameshazungumza na Kaimu Meneja wa Mkoa, Kahitwa Bishaija kuhusu, kuongeza transfoma zingine kwa sababu kwa sasa Kituo cha Zuzu Dodoma baada ya kuondolewa kwa transfoma hiyo waliyoichukua na kupeleka Morogoro hakuna nyingine iliyobaki na kwamba litapotokea tatizo kwingine itakuwa ni shida.

Aidha, alisema wanajipanga kuanza kufanya tathmini ya gharama za transfoma zilizoharibika kimatengenezo ili wazifanyie maamuzi kama wanunue mpya au wazifanyie marekebisho kwa sababu ya uwapo wa transfoma kubwa nyingi zilizoharibika ikiwamo aina ya 20MVA na 6MVA kwenye vituo vyao mbalimbali nchini.

Hata hivyo, alisema wameshaanza mazungumzo na Korea ili kutafuta vifaa vya kurekebisha mitambo na kazi kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Pia alisema walifanya tathmini ya ukuaji wa mahitaji ya umeme kwa kila mkoa na kwamba kwa miaka mitano ijayo zitahitajika ziada ya megawatt 1,000 kwa mikoa yote na kwamba wana mpango wa kuongeza kituo kingine mwaka huu mkoani Morogoro kwa kuwa ni mkubwa na una matumizi makubwa ya uzalishaji wa chakula na mazao ya mengine.

## Marufuku ya kutoishi na watoto kisiwani yapaza sauti za wazazi

**Na Richard Makore,** MWANZA

MARUFUKU iliyotolewa mwaka juzi na uongozi wa kisiwa cha Kome wilayani Sengerema Mkoa wa Mwanza kuwazuia wazazi kutoishi na watoto wao imelalamikiwa na wakazi hao.

Zaidi ya wakazi 3,000 katika kisiwa hicho walipigwa marufuku na serikali kuishi na watoto wao maeneo hayo, kutokana kukosekana kwa huduma muhimu za kijamii na uwapo wa mamba.

Katika mahojiano maalum na Nipashe yaliyofanyika juzi kwa njia ya simu, Mwenyekiti wa Mwalo wa wavuvi wa Mchangani kisiwani humo, Revocatus Chuwa, alisema mpaka sasa hawafahamu watoto hao watakuwa wa aina gani kutokana na kuishi nao mbali katika malezi.

Chuwa alikiri kuwa eneo hilo halina huduma muhimu kama shule, afya na hawana kituo cha polisi kilicho karibu yao.

"Tunaishi kama wanyama na nina hakika tutazalisha kizazi kibaya kwa sababu wazazi hawaruhusi kuishi na watoto, kitendo ambacho ninakiona kama kitavuruga maisha ya watoto," alisema. Alibainisha kuwa baadhi ya wazazi wanalazimika kutafuta wafanyakazi na kuwapangia nyumba wilayani Sengerema au jijini Mwanza ili wawasaidie kukaa na watoto hao.

Alisema kwa wale ambao hawamudu kufanya hivyo, wanalazima kuwapeleka watoto wao kwa majirani au ndugu yeyote na wao kurudi kisiwani humo kuendelea na shughuli za uvuvi.

"Hatuna huduma muhimu za kijamii ila Serikali inakusanya mapato yake kila mwezi, kila mtu aliyejenga kibanda cha kuishi analazimika kukilipia kati ya Sh. 3, 000 hadi 6,000 na kwa mwalo mzima kuna vibanda zaidi ya 6, 000, tumekuwa tukiwaona watumishi wa serikali wanakuja kukusanya mapato yatokanayo na samaki," alisema Chuwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Julius Mulongo, anathibitisha kukosekana kwa huduma muhimu katika eneo hilo, lakini anaeleza ,hajapata taarifa rasmi za kimaandishi kutoka viongozi wa eneo hilo ili wazifanyie kazi.

Eneo hilo ambalo zinafanyika shughuli za uvuvi, wakazi wake wanachangia mapato ya Halmashauri ya Sengerema yanayofikia Sh. milioni 15 kwa kila mwezi.

## Tigo yajipanga kuhamia makao makuu mapya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo imetia saini mkataba wa kupanga jengo la PSSSF Commecial Complex kwa lengo la kuziweka sehemu moja timu zilizounganishwa za Tigo na Zantel.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tigo CPA, Innocent Rwetabura, alisema lengo lingine ni kujenga mazingira bora yatakayochagiza umoja na ubunifu miongoni mwa wafanyakazi wao ili kwa pamoja kutengeneza bidhaa na kutoa huduma za hali ya juu kwa wateja zaidi ya milioni 14 kote nchini.

"Tunatarajia kuhamia mwishoni wa mwaka huu. Ofisi hizi mpya zitaakisi utamaduni wa taasisi iliyounganishwa ya Tigo na Zantel, na tutajitahidi kuifanya iwe mahali pazuri pa kufanya kazi na kukuza vipipaji vya ndani," alisema Rwetabura.

Alisema, makazi hayo mapya yanajumuisha vyumba vya mikutano vilivyowezeshwa na teknolojia na vituo vya kazi ambapo wafanyakazi wa Dar es Salaam na wa nje ua Dar es Salaam na wadau mbalimbali wataweza kutimiza majukumu yao kikamilifu.

"Kampuni ya Tigo imekuwa mstari wa mbele katika kubuni bidhaa na huduma zinazowalenga mteja mmoja mmoja pamoja na wateja wa kampuni kubwa na madogo," alisema.

Alifafanua kuwa uhamishaji wa makao makuu ya Tigo Tanzania kutoka jengo la Derm Complex Kijitonyama hadi PSSSF Commercial Complex hakutaathiri utoaji wa hautaathiri utoaji wa huduma zao

"Niwashukuru tena wenyeji wetu PSSSF kwa kutupa ushirikiano wa hali ya juu na kuhakikisha zoezi hili linafanyika kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya pekee nichukue fursa hii tena kumshukuru kwa dhati Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, CPA Hosea Kishimba, kwa kuwa nasi kila hatua na kuhakikisha tunafanikisha siku hii ya utiaji saini," alisema.

Rwetabura pia aliwashukuru aliwashukuru wafanyakazi wa Tigo walioshiriki kikamilifu katika mchakato wa utafutaji wa jengo hilo na wale wote walioshiriki katika hatua zote za kutayarisha mkataba huo.

# Mtandao wataka wanawake wasaidiwe kutatuliwa vikwazo vinavyowakabili

**Na Mwandishi Wetu ,**
PEMBA

WANAMTANDAO wa kuibua changamoto zinazowakabili wanawake kisiwani Pemba (citizen briged) wamesema iwapo changamoto walizoziibua zitatatuliwa, wanaamini itasaidia sana kuamsha ari kwa wanawake kuombea nafasi za uongozi ifikapo 2025.

Wanamtandao hao walisema wanawake wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali ndani ya jamii zao ambazo husababisha muda mwingi kuzifikiria na kukosa uwezo wa kufikiri namna gani wanaweza kuingia katika uongozi. Wakizungumza wakati wa mkutano wa kuwasilisha ripoti ya miezi mitatu huko Chake Chake, wanamtandao hao walisema,= changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama, huduma ya umeme, vituo vya afya, vyeti vya kuzaliwa, ukosefu wa vyoo mashuleni na hali ngumu za maisha, ndizo zinazowakamisha wanawake kugombea nafasi za uongozi.

Mmoja wa wanamtandao hao, Hamad Omar Khamis kutoka Wilaya ya Wete, alisema kwa miezi mitatu walifanikiwa kwenda kwenye shehia za Mchangamdogo, Kojani na Pembeni, ambapo waligundua familia zinazoishi mazingira magumu na kushindwa hata kumiliki sare za shule za watoto wao.

"Tulipita baadhi ya shehia na kuibua changamoto na tulizifikisha taasisi husika, hivyo tunaziomba taasisi hizo kuchukua hatua za haraka ili kumsaidia mwanamke aweze kushiriki katika nafasi za uongozi," alisema.

"Changamoto zipo nyingi na tayari tumeshazifikisha Serikalini, hivyo tunaomba zitatuliwe ili kumuondoshea mwanamke kikwazo cha kutokugombea," aliongeza.

Maryam Hemed Said wa Wilaya ya Micheweni, alisema kuwa walifanya kazi ya utetezi na kutoa ushauri katika shehia za Mihogoni na Shumba vyamboni, pamoja na kutoa mwamko kuhusu umuhimu wa demokrasia na uchaguzi, huku wakiendelea kuibua changamoto.

Alieleza kuwa kuwapo kwa taarifa zisizo sahihi kwenye vitambulisho vyao, ni jambo linalowakosesha haki zao za msingi ikiwmo mafao ya uzeeni.

Ali Abdalla Juma wa Wilaya ya Chake Chake, alisema miongoni mwa changamoto walizoziibua ni kuzurura ovyo kwa wanafunzi wanaokaa shule ya bweni ya Sekondari Madungu huku wanafunzi wa shule ya Shamiani kuchelewa kwenda shuleni kupita kiasi.

Mkurugenzi wa PEGAO Pemba, Hafidh Abdi Said, alisema ushirikiano unahitajika katika kuendelea kuzifuatilia changamoto walizoziibua ili kuhakikisha zinapatiwa ufumbuzi unaofaa.

Mratibu wa mradi huo, Dina Juma Makota, aliwataka wanamtandao hao kuzifanyia kazi kwa pamoja changamoto hizo ili kuhakikisha wanamuondoleoa vikwazo mwanamke aweze kugombea nafasi za uongozi.




Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga akizungumza na waandishi wa habari jana, (hawapo pichani) alipotoa tamko la kituo hicho la kulaani jaribio la kutaka kukatwa mkono Mohamed Rajabu, mwenye ualbino. Kushoto ni Ofisa Programu Maduhu William na Mkurugenzi Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji Felista Mauya. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanafunzi wapewa elimu dhidi ya malaria

**Na Romana Mallya**

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi AgaKhan jijini Dar es Salaam, wamepatiwa elimu ya malaria na Kampuni ya Bima ya Jubilee Health Insurance kwa lengo la kuwawezesha watoto hao kujilinda pamoja na familia zao dhidi ya ugonjwa huo.

Meneja wa kampuni hiyo anayehusika na Huduma kwa Wateja, Veronica Nyange akizungumza na waandishi wa habari shuleni hapo jana jijini Dar es Salaam ikiwa ni Siku ya maadhimisho ya Malaria Duniani, alisema wameamua kutoa elimu kwa wanafunzi ili waweze kujilinda na mbu wanaoeneza ugonjwa huo.

Alisema wanawaelekeza njia za kujilinda wao na familia zao dhidi ya ugonjwa huo na kuwaelekeza tiba zake.

"Hatutaishia hapa tutakwenda maeneo mbalimbali kutoa elimu ya Malaria ili jamii iweze kufahamu njia zipi wanapaswa kuzichukua kujilinda na ugonjwa huu. Leo tunawapatia wanafunzi vifaa vya kujikinga na mbu", alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Awali na Msingi AgaKhan, Blandina Duwe alisema wamekuwa wakiwaeleza mara kwa mara wanafunzi athari za kuumwa na mbu aenezae malaria.

"Mara nyingi watoto hasa nyakati za mchana wanapong'atwa na mbu hutaka kujua amekang'atwa na mbu je, ana Malaria, maswali kama haya yanapokuja kwetu huwa tunawaelimisha kwamba yupo mbu maalum ambaye anaambukiza Malaria na tunawaeleza ili mtu awe nayo hupitia dalili mbalimbali na atakapopimwa na mtaalam wa afya atathibitisha kuwa ana malaria au la na kupewa tiba muafaka," alisema.

Pia alisema huwaelimisha matumizi ya vyandarua, kusafisha mazingira yao ya nyumbani ili kutokomeza mazalia ya mbu na wadudu wengineo.

Pia alisema kwa upande wa Shule kila mara wamekuwa wakinyunyiza dawa kwa lengo la kukabiliana na wadudu wa aina zote wakiwamo mbu.

Mwanafunzi wa darasa la tano shuleni hapo, Giana Rwanyakato, alisema anafahamu kuwa malaria inaenezwa na mbu hivyo akiwa nyumbani familia huakikisha inafunga madirisha na milango na hutumia chandarua ili kujiepusha kung'atwa na mbu.

"Ujumbe wangu kwa leo ikiwa ni siku ya Malaria duniani, familia zichukue hatua kusafisha mazingira kwa sababu mtu aking'ata na mbu anaweza kupata Malaria, mkiwa nyumbani fungeni madirisha na milango na mnunue chandarua na dawa za kuangamiza mbu," alisema.

Daktari Romana Malikusema ambaye anashirikiana na Kampuni ya Jubilee kutoa elimu hiyo alisema ugonjwa wa Malaria mpaka sasa ni tishio unaua kwa haraka endapo matibabu stahiki hayatafanyika.

Alisema kwa kushirikiana na timu ya Jubilee Insurance wamefika shuleni hapo kutoa elimu kwa wanafunzi kwa sababu wanaamini kila mwanafunzi ana ndoto zake na anataka kuzifikia.



Wabunge wakisaini kitabu cha maombolezo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa, Marehemu Irene Alex katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Mkandarasi Stendi ya Magufuli asamehewa kodi ununuzi vifaa

SERIKALI imesema imeshatoa msamaha wa kodi kwa mkandarasi wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha mabasi cha Magufuli mkoani Dar es Salaam kwa ajili ya ununuzi wa vifaa ili kukamilisha ujenzi huo ifikapo Juni mwaka 2022.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Festo Dugange alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibamba (CCM), Issa Mtemvu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini ujenzi wa Kituo hicho utakamilika kwa asilimia 100 na serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kituo hicho kinafanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Akijibu swali hilo, Dk.Dugange alisema Kituo hicho kinachoendelea na ujenzi katika eneo la Mbezi Luiz kilianza ujenzi Januari, ,mwaka 2019 kwa mkataba wa miezi 18, hivyo ujenzi ulipaswa kukamilika Julai, 2020.

“Mkandarasi aliongezewa muda wa ujenzi hadi Juni, 2022 kutokana na kuchelewa kutolewa kwa msamaha wa kodi wa vifaa vya ukamilishaji wa ujenzi huo,”alisema.

Alibainisha kuwa hadi Machi, 2022 Sh. bilioni 53.09 sawa na asilimia 94.73 zilikuwa zimelipwa kukamilisha ujenzi.

“Aidha, Machi, mwaka 2022 serikali imetoa msamaha wa kodi na sasa mkandarasi anaendelea na manunuzi ya vifaa ili kazi ya ujenzi iendelee na kukamilika ifikapo Juni, 2022,” alisema.

Naibu Waziri huyo alisema kukamilika kwa kazi hizo kutafanya kituo hicho kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.




Habari zote na Augusta Njoji

# Uhaba watumishi waathiri huduma kituo cha afya

BUNGE limeelezwa kuwa Kituo cha Afya Nanyara mkoani Songwe tangu kijengwe ni miaka mine, lakini hakuna watumishi wa kutosha kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Akiuliza swali bungeni, Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga, alihoji mkakati wa serikali kupeleka wafanyakazi katika kituo hicho.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk.Festo Dugange, alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha kituo kinakuwa na watumishi wa kutosha na watapelekwa ili kutoa huduma za afya.

Hivi karibuni, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ilitangaza ajira zaidi ya 17,000 zikiwemo za kada za mbalimbali za afya 7,612.

Hadi kufikia Aprili 25, mwaka huu, maombi ya ajira yaliyopekelewa kikamilifu kwa kada ya Afya ualimu ni 83,514 kwa siku tano ikiwa ni wastani wa waombaji 16,703 kwa siku.

# Chikota ataka lami barabara Mtwara-Songea

MBUNGE wa Nanyamba, Abdallah Chikota (CCM), ameomba serikali kutenga fedha za dharura kwa ajili ya kujenga angalau kilomita 70 kwa kiwango cha lami barabara ya Mtwara-Newala-Masasi hadi Songea kutokana na umuhimu wake kiusalama.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni, Chikota alisema ni vyema serikali ikafanya jitihada za haraka za kuimarisha barabara hiyo ambayo ni muhimu katika suala zima la usalama.

“Naomba kujua ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya ulinzi kutoka Mtwara-Newala-Masasi hadi Songea Kwa kiwango cha lami?”

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya akijibu maswali hayo, alisema barabara ya ulinzi ya kutoka Mtwara - Newala - Masasi hadi Songea yenye urefu wa kilometa 358, inaambaa na Mto Ruvuma.

“Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa inaendelea kuifungua barabara hii kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja makubwa na madogo katika mito na mikondo ya maji inayokatisha barabara hii iliweze kupitika,”alisema.

Alisema kilometa 208 zimefunguliwa na daraja kubwa la Mbangala (mita 120) mkataba wa ujenzi ulisainiwa 11 Aprili, 2022 na baada ya kuifungua barabara yote Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

# Matiko ahoji ujenzi soko kutokamilika

MBUNGE wa Viti Maalum, Esther Matiko, ametaka kujua sababu za Serikali kushindwa kukamilisha ujenzi wa soko la kimkakati la Kimataifa la Remagwe.

Akiuliza swali hilo bungeni jana, Matiko alisema soko hilo limetelekezwa kwa takribani miaka 10 na kuhoji kwanini serikali haikutenga bajeti kila mwaka ili kukamilisha mradi huo.

“Mkoa wa Mara unazalisha mazao ya chakula na mifugo kulisha ndani ya nchi na kuuza nchi jirani ya Kenya lakini wakulima hawa wanauza kwa bei chee ni kwanini sasa serikali isione umuhimu wa dharura wa kukamilisha soko hili la kimkakati ili kutatua tatizo la masoko kwa wakulima?”alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko ya Kimataifa ya kimkakati kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo nje ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

“Serikali iliamua kuanzisha masoko ya kimkakati ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa soko la Remagwe katika mpaka wa Sirari chini ya Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo Wilayani yaani District Agricultural Sector Investment Project (DASIP) uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB),”alisema.

Alisema serikali inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha soko hilo.

“Tumewaambia wenzetu katika Halmashauri kuanza kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya kujenga masoko haya, kwa anachokisema serikali imekuwa ikifanya na kuhakikisha masoko yanakamilika kama inavyotakiwa,”alisema.

ama
ALHAMISI APRILI 28, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**MGANGA MFAWIDHI:** Hospitali Shinyanga ipo shida kutibu wenye ulemavu kusikia



Ukurasa 13

Zanzibar yadumisha rekodi ya dunia, idadi ya maambukizi ikikaribia sifuri



Ukurasa 14

**Ujasiri wa kiuchumi anaoenda nao Rais Samia, wajibu aungwe mkono**

AFYA

# Serikali inapokuja na orodha ya mikakati kufuta mimba utotoni

**Na Yasmine Protace**

MIKAKATI inapoanzishwa na kusimamiwa vizuri katika sehemu husika, huwa daima inazaa matunda.

Hivi karibuni katika kikao kazi kati ya waandishi wa habari na wizara, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Catherine Sungura, ameainisha Sera ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2007, ikiwa na maudhui ya kisera na kwa afya ya jamii.

Anasema, kwa sasa kuna mafanikio makubwa ikiwamo programu za Mabusha, Malaria, HIV na Matende, akidokeza: "Sera ya Afya ya Mwaka 2007 tulikuwa tunasimamia tamko la kisera linalozungumzia kuboresha afya."

Pia, anasema kumekuwapo maboresho makubwa, ikiwamo upatikanaji wa vifaa tiba na dawa, akiongeza kuwa wameshafanikiwa kuboresha miundombinu na upatikanaji madaktari bingwa, kuendana na maboresho makubwa ya sasa.

Lingine anallityaja ni maboresho katika eneo la utalii, matibabu na kuwapo bima ya afya kwa wote. Hapo Catherine anafafanua namna Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, inayoandaliwa sasa, inavyofafanua huduma za afya zinavyopaswa kuwa katika ngazi zote, kuanzia zahanati, vituo afya hadi hospitali za wilaya.

Anasema, fedha zitokakanazo na Uvico zimesaidia kuboresha huduma nyinginezo hospitalini, zahanati na vituo vya afya, akirejea Mkakati wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano, kwa hospitali za rufani kila mkoa, kunalengwa kuwapo huduma za kibingwa hadi ngazi ya kila kata.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Profesa Abel Makubi. **PICHA: MTANDAO**

"Tunapenda kila eneo tunataka huduma ziwe zinatolewa, tofauti kuendana na changamoto zilizopo," anasema.

Mtaalamu huyo anataja Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya ulioanza kutekelezwa mwaka jana na kwisha 2026, unadhamiria kuweka wadau wa afya pamoja katika kutoa huduma.

Anataja mkakati mwingine, namna huduma ya mama na mtoto kupunguza vifo vya uzazi ifikapo mwaka 2025, kwa wastani kutoka vifo vya vizazi 250 vya sasa hadi 100, kwa kila watu 100,000.

Cathetrine anasema, pia wameendelea kuboresha miundombinu hata kwa mama anapojifungua na kupata tatizo, anapata huduma na mtoto, pia anaendelea kulindwa kuwa hai na salama.

**KUPUNGUZA VIFO**

Mtaalamu huyo anaeleza kwamba, katika kupunguza vifo vya watoto wachanga, kuna mpango umewekwa kuanzia mwaka jana hadi 2025, ikiwa ni sehemu ya kuwanusuru.

Anaeleza mkakati mwingine, unagusa kupunguza vifo vya watoto chini chini ya miaka mitano, kutoka vifo 50 hadi watoto 38.

Catherine anataja mkakati mwingine unalenga kupunguza mimba za utotoni kwa wasichana, kutoka asilimia 50, lengo ni kudhibiti vifo vya watoto na mama zao, Kitengo cha Afya ya Uzazi, kikibebeshwa jukumu la kunusuru.

Anasema katika kutoa elimu kwa vijanam, wanashirikiana na wadau ili waweze kuzifikia rika za vijana wakijitambua pasipo kuwa mbali na mimba.

Pia, Catherine anataja mkakati mwingine unaagukia kupunguza vifo vitokanavyo na maambukizi ya Ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, akidokeza kuwapo sheria muhimu zinazoangaza afya ya jamii kuanzishwa maabara na mfuko wa bima ya afya kwa wote.

Ofisa huyo wa afya, anasema katika kipindi cha mwaka mmoja, wameweza kujitangaza na kuboresha huduma za matibabu kwa mteja, pia upatikanaji wa dawa.

Catherine wanawasisitiza watoa huduma za afya, wawe wafanisi katika kutoa huduma sahihi kwa wagonjwa wanaofika kupata matibabu, akiamini unapoendana na uwezeshaji, kusaidia uondoaji shida na tiba njema.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, wanaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi, ikiwamo kuwafadhili watoa huduma kupata mafunzo.

Pia, anataja mkakati wa Sheria na Sera ya Bima ya Afya kwa wote, ikiwamo kupambana na magonjwa yasiyokauambukiza.

Cathetrine anaeleza la muhimu, kuhamasisha jamii iache tabia ya kula vyakula bila ya kufanya mazoezi, huku serikali ikiwa na mkakati mwingine wa kuongeza bajeti katika sekta ya afya, ikiboresha ushirikiano na wadau wa afya ndani na nje ya nchi.

AFYA

# Mganga Mfawidhi: Hospitali Shinyanga ipo shida kutibu wenye ulemavu kusikia

• SHIVYAWAYA wakiri ni kundi linalotaabika zaidi



Sehemu ya Hospitali ya Rufani Shinyanga. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATU wenye ulemavu wa kusikia (viziwi) na kuongea (bubu), wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi katika kupata huduma za kijamii, zikiwamo za afya, wanashindwa kuwasiliana vyema na wahusika kwa kutoelewana lugha.

Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, nayo inakabiliwa na ukosefu wa wataalamu wa lugha za alama, wanaopaswa kufanya kazi ya kutasfiri kwa wagonjwa wenye ulemavu wa kusikia na kuongea, ili madaktari na wauguzi watambue ugonjwa unaowasumbua na kuwapatia tiba sahihi.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa Shinyanga, Dk. Luzila John, anasema hawana mkalimani wa lugha za alama, hata kuwapa shida kwenye utoaji huduma ya matibabu kwa wenye ulemavu wa kusikia na kuongeza sababu ya ukosefu wa mawasiliano.

Anasema wanapopata wagonjwa wenye ulemavu wa kusikia na kuongea hospitalini hapo, huwa wanapata tabu ya kuchukua taarifa zao kujua namna wanasumbuliwa na tatizo gani na kuamua kutumia lugha ya ishara, hata wakawapatia matibabu kwa kutumia uzoefu.

"Tunapata shida sana ya kutoa matibabu kwa watu wenye ulemavu wanapofika kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, lakini watumishi wetu huwa wanajitahidi kuelewana nao hivyo hivyo kwa kutumia ishara na kuwapatia tiba.

> **Ninachokiomba kwa watu hawa wenye ulemavu, wanapokuja kupatiwa matibabu hospitalini hapa waje na wakalimani wao, pamoja na vielelezo ya utambulisho wao, ili iwe virahisi kupata maelezo yao na kuwapatia tiba stahiki.**

"Ninachokiomba kwa watu hawa wenye ulemavu, wanapokuja kupatiwa matibabu hospitalini hapa waje na wakalimani wao, pamoja na vielelezo ya utambulisho wao, ili iwe virahisi kupata maelezo yao na kuwapatia tiba stahiki," anaongeza Dk. John.

Anaeleza kuwa kama kuna uwezekano wa taasisi au mashirika, ambayo yanajihusiha na wenye ulemavu wafike hospitalini hapo na kutoa elimu ya lugha za alama kwa watumishi, ili waitambue lugha hiyo walau hata kidogo na kuwasaidia kutoa tiba sahihi kwa watu wenye ulemavu.

### OFISA USTAWI JAMII

Ofisa Ustawi wa Jamii katika Hospitali ya Rufani Shinyanga, Prisla Mushi anayehusika na mapokezi ya wagonjwa hospitalini hapo, anasema wanapotaka wagonjwa wenye ulemavu wa kusikia na kuongea, hushindwa kuelewana nao, kwa kuchukua taarifa zao za ugonjwa na kuziwasilisha kwa daktari.

Anasema kwa kutofahamu lugha za alama, huwa wanajaribu kuwasiliana nao kwa ishara, pamoja na kuwaandikia kwenye karatasi kwa wanaojua kusoma na huwajibu, hata kupata taarifa zao, lakini wasiojua kusoma ndiyo hubaki na changamoto wakashindwa kuelewana.

"Mgonjwa yeyote akija hosptalini hapa, lazima aanze kufikia kwetu kitengo cha mapokezi na kuchukua taarifa zao zote ndipo aende kwa daktari kupata matibabu. Sasa wanapokuja wagonjwa wenye ulemavu wa kusikia na kuongea, huwa tunapata shida sana ya mawasiliano, kwa sababu hatukujua lugha za alama.



Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John.

"Kitu ambacho huwa tunakifanya ni kuwasiliana nao kwa ishara na kupata taarifa zao. Kwa wale ambao wanajua kusoma, huwa hatupati shida sana, tatizo kubwa ni wale ambao hawana elimu na wakati mwingine huwa tunashindwa kabisa kuelewana na kushindwa kuwatibu," anaeleza.

Kwa mujibu wa Mushi, kuna wakati wanashindwa hata kuelewana na mgonjwa mwenye ulemavu wa kuongea, hata wakati wanafika hatua kugadhabika wakafanya fujo hospitalini, sababu kuu ni pale inakuwa vigumu kupata taarifa zao kubaini ugonjwa unaomsumbua. Hapo inabidi apatikane mkalimani anayewasaidia.

Anasema katika kipindi cha nyuma kati ya mwaka 2013 na 2014, baadhi ya watumishi hospitalini hapo walipatiwa elimu ya lugha za alama na walikuwa msaada mkubwa kwa wagonjwa wenye ulemavu, lakini sasa wote hao hawapo, hivyo anaomba elimu itolew kila wakati hata kuwawezesha kutoa tiba stahiki kwa wenye ulemavu.

### MTAALAMU LUGHA

Kambuli Pius, ni mtaalamu wa lugha za alama mkoani Shinyanga, anayesema mkoani humo wanaojua lugha hizo ni wachache, isipokuwa zaidi kwenye shule jumuishi na mara nyingi, yeye ndiyo huwa wanamtumia sana kutoa uainishi huo wa lugha za alama kwa wenye ulemavu.

Anataja sehemu wanakopata changamoto, ni eneo la huduma za afya, kwa sababu wauguzi na madaktari whawana uelewa wa kutosha kuhusu lugha ya alama, hata wanaposhindwa kuelewana na mgonjwa, huwa wanamuita kwenda kusaidia ukalimani wa lugha.

"Wataalamu wa lugha za alama wapo wachache sana Shinyanga, mfano mimi huwa nahudumu karibia mkoa mzima. Ndiyo maana hivi karibuni natarajia kuanzisha kituo cha kutoa mafunzo ya lugha za alama kwa watu wote, wakiwamo watumishi wa serikali.

"Wataalamu wa kukalimani lugha za alama tukiwa wengi mkoani hapa, pamoja na watumishi wa serikali kuijua lugha hii, itasaidia kwa kiasi kikubwa watu wenye ulemavu kupata mahitaji yao muhimu, kwa sababu hakutakuwa na kizuizi tena cha mawasiliano," anaongeza Pius.

### KUTOKA SHIVYAWATA

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA) Richard Mpongo, anakiri wenye ulemavu hasa wa kusikia (viziwi) na kuongea (bubu), wamekuwa wakipata shida ya kupata huduma za afya, kutokana na kushindwa kuelewana lugha na watumishi.

"Ili kuelewana na mtu mwenye ulemavu wa kusikia au kuongea, inahitaji upate walau hata kidogo mafunzo ya lugha za alama, tofauti na hapo kuelewana ni vigumu," anasema Mpongo.

Anaiomba serikali iwapeleke wataalamu wa kukalimani lugha za alama kwenye huduma hizo za kiafya, maeneo anayoyasema ni muhimu sana katika kuokoa afya zao, ili wanapoenda kupatiwa matibabu wapate kuelewana na wataalamu na kupata tiba sahihi.

AFYA

MAADHIMISHO SIKU YA MALARIA

# Zanzibar yadumisha rekodi ya dunia, idadi ya maambukizi ikikaribia sifuri

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

• Inatiwa doa na wasafiri wake; Lengo mwakani ibaki historia

ZANZIBAR ni kati ya maeneo duniani yaliyofanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza maambukizi ya malaria. Wastani wa watu 100 wanaopimwa vimelea vyake haizidi mtu mmoja anayekutwa nao.

Waziri wa Afya Nassor Ahmed Mazrui, anatahadharisha, ahueni hiyo haimaanishi ugonjwa umemalizwa Zanzibar, ikiwamo maambukizi kutoka kwa wasafiri.

Juzi April 25, dunia imeadhimisha Siku ya Malaria Duniani, huku Zanzibar kimtaifa kukitajwa kupo katika hali nzuri. Takwimu za Wizara ya Afya kwa miaka 10 sasa zinaonyesha tatizo la malaria liko chini ya asilimia moja.

Waziri Mazrui anasema, takwimu za mwaka jana zinaonyesha wagonjwa 6096 walioripotiwa na kuthibitishwa kuugua malaria. Katika hilo, anarejea wastani wa kijinsia,wanawake walikuwa 2,377 (39%) na wanaume 3719 (61%). Mgawanyo huo katika tafsiri ya kawaida, kinamama walikuwa theluthi moja, huku kinababa ni theluthi mbili.

Pia, kutoka jumla hiyo kuu, watoto waliogua na wana umri chini ya miaka mitano walikuwa 549, ambao ni sawa na asilimia tisa.



Ofisa Mfuatiliaji wa Wagonjwa wa Malaria, Faki Mlekwa Faki, akimhudumia mgonjwa wa malaria, Mwanaidi Rashidi, katika kijiji cha Ghana, Wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

### HALI YA WASAFIRI

Mazrui anasema, ugonjwa huo kwa wasafiri wa ndani kati ya Unguja na Dar es Saalam na mikoa ya Tanzania Bara, bado ni changamoto inayohitaji msaada mkubwa, hasa ikizingatiwa Zanzibar ina bandari nyingi zisizo rasmi.

"Wapo wasafiri wanaotumia bandari zisizo rasmi kusafiri kutoka Unguja kwenda Tanzania Bara, baadhi yao hukutwa na maambukizi ya ugonjwa huo," anasema Waziri Mazrui.

Anafafanua takwimu za wizarani kwake zinaonyesha kati ya wagonjwa 6,096 walioripotiwa mwaka jana, wapo 4,145 sawa na asilimia 68 wana historia ya kusafiri nje katika maeneo tofauti ya Tanzania Bara.

Waziri Mazrui anasema, mwaka jana kulikuwapo vifo vinne vitokanavyo na malaria, huku akitamka lengo la mwaka ujao ni kufuta kabisa maambukizi hayo.

Kwa mujibu wa mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Zanzibar ni miongoni mwa maeneo yanayokaribia kutokomzea malaria kwa wakazi wake.

"Ugonjwa wa malaria unaambukizwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine baada ya kusambazwa na mbu," anaeleza waziri, anayetaja kaulimbiu ya mwaka huu ni: "Ewe msafiri, chukua tahadhari Zanzibar ibaki bila ya 'Malaria Zero' malaria inaanza na mimi."

### WILAYA ZENYE USUGU

Meneja Programu wa Kumaliza Malaria kutoka Kitengo cha malaria Zanzibar, Muhammed Ali Abdallah, anasema taarifa zinaonyesha Wilaya za Magharibi 'A'na 'B, pia Wilaya Kati Unguja, ndizo zinazoongoza kuripoti wagonjwa wengi zaidi.

"Hii inaamanisha kuwa maambukizi ya ugonjwa huu bado yanaendelea ndani ya wilaya hizi. Kwa mnasaba huu, wizara imo katika matayarisho ya kuendesha zoezi la upigaji dawa shehia zote za wilaya hizo kwa utaratibu utakaotolewa na wataalamu," anasema.

Anasema Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Malaria, inaendelea kusisitiza matumizi ya mikakati ya kupambana na malaria, ikinyesha mafanikio makubwa.

Pia, anasitiza matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa; tiba sahihi yenye dawa mchanganyiko; kushiriki upigaji dawa majumbani katika maeneo maalum; na kusimamia usafi wa mazingira, lengo ni kuondosha mazalia ya mbu na kuwatumia Wahudumu wa Afya ya Jamii Ngazi ya Shehia (CHV).

"Katika kuhakikisha mikakati hii inafanikiwa Wizara ya Afya kwa mwaka 2021 kupitia vituo vya afya 180, imegawa bila ya malipo jumla ya vyandarua 165,140 kwa mama ya wajawazito, watoto mwenye umri miezi tisa na wanajamii kutoka Shehia zote 383 za Unguja na Pemba," anasema.

### KAMPENI ZINAVYOENDELEA

Meneja Progamu Abdallah, anafafanua kuwapo vyandarua vilivyotiwa dawa 727,872 vilivyotolewa katika shehia 335 za Unguja na Pemba, kisaidia kujikinga dhidi ya malaria.

Taarifa za utafiti kutoka Wiazra ya Afya, kuhusu uelewa na huduma za malaria mwaka 2021, ulionyesha matumizi ya vyandarua kwa jamii yameongezeka kutoka asilimia 73 za mwaka 2020 hadi asilimia 85 mwaka 2021.

Pia, utafiti unafafanua kati ya nyumba 49,235 zilizoorozedheshwa mafanikio, zipo 46,313 sawa na asilimia 94.1 zilipigwa dawa za kuua mbu wa malaria na wizara inaendelea kupiga dawa katika maeneo yanayoripotowa kuwapo wagonjwa wengi yenye sura ya mlipuko.

Inaelezwa, kuanzia Januari hadi mwezi huu, nyumba 18,697 (95.9%) kati ya 19,359 zilizolengwa kutoka Shehia 37 za Unguja na Pemba, zimepigwa dawa ya kuua mbu wa malaria.

Safia Muhammed, Ofisa Uchunguzi wa Vimelia vya Malaria, anadem wana vifaa vya upimaji wa malaria katika Bandari ya Malindi Unguja na viwanja vya ndege, zinazowawezesha wasafiri kupima vimelea, hata wakadhibiti maambukizi mapya.

> Wapo wasafiri wanaotumia bandari zisizo rasmi kusafiri kutoka Unguja kwenda Tanzania Bara, baadhi yao hukutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Anafafanua: "Suala la kupima malaria kwa wasafiri ni hiyari, hivyo wasafiri huhamasishwa wapime na kwa mwaka 2021 wasafiri 11 waligundulika kuwa na malaria baada ya kupimwa."

Safia ansema, maambukizi yamehama kutoka Kwa watoto umri chini ya miaka, kwa sababu bado ni wanufaika wa vyandarua.

Juma Hassan Mcha, ni Mdhibiti Mbu katika Kitengo cha Kudhibiti Malaria, anasema baada ya kuwepo malalamiko kuhusu dawa ya kuulia mbu majumbani iliyokuwa ikitumika kuwa na athari kwa jamii iliwemo uwasho, sasa imebadilisha.

### ANAYOSHUHDIA TABIBU

Mganga katika Kituo cha Afya, Kianga, wilaya ya Magharib 'A' Unguja, Dk. Salma Muhammed Hemed, anasema kuna jumla wagonjwa 1500 waliopimwa malaria mwaka jana, kati yao 23 waligundulika kuwa nayo, 20 walikuwa wasafiri watokao Unguja kwenda Tanzania Bara.

Anasema kituoni hapo wanakinga na tiba ya malaria ikiwamo matumizi ya dawa kwa mgonjwa wa malaria na utoaji vyandarua kwa watoto na mama wajawazito, ili kujikinga na ugonjwa huo.

Daktari wa Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini Unguja, Juma Ali Makame, anasema elimu wanayoitoa kituoni kuhusu malaria memesadia kupunguza wagonjwa kituoni hapo.

Anafafanuia kuwa, wametoka wagonjwa 546 waliopimwa mwezi Januari mwaka huu, hadi walikutwa na malaria na kupatiwa matibabu; Febuari walipimwa watu 330 na 12 walikutwa na malaria; huku mwezi Machi wagonjwa tisa walikutwa na malariam kati ya 317 waliopimwa.

"Tukilinganisha na tulipotoka hii idadi ya wagonjwa wa malaria ni ndogo sana kwa hospitali yetu hii ya wilaya, kwa sababu elimu ya afya ya kujikinga na malaria imesaidia sana kupunguza idadi ya wagonjwa hao," anasema.

Mkuu wa Kituo cha Afya Kidimni, Wilaya ya Kati Unguja, Dk. Rajab Haji Rajab, anasema kituo hapo wanaibua wagonjwa wengi wa malaria, akidokeza mwezi huu ukobakiza siku mbili kumalizika, wamewaibua wagonjwa watatu wa malaria,wote wasafiri.

Faki Mlekwa Faki, ni Ofisa Mfuatiliaji wa Wagonjwa wa Malaria Wilaya ya Kati Unguja, anasema anawafuatilia wagonjwa wote wanaofika hospitali na kugundulika malaria, pia akiwatibu hata majumban, ili kudhibiti maambukizi yasiendelee.

Anasema, ni aina ya mfumo ulioorahisisha kuwajua wanaougua, hata wakawafuatilia.

# Ujasiri wa kiuchumi anaoenda nao Rais Samia, wajibu aungwe mkono

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI umefika ili utalii wetu upanuke zaidi, tunahitaji jasiri wa kusimamia, tena si kwa kutoa majibu mepesi, mbele ya taasisi inayohitaji majaibu huru.

Kwa zama iliyopo sasa, tena kwa kwa utitiri ulioko wa vyombo vya habari mitandao ya mawasiliano ilyozagaa kushindwa kutangaza vivutio vyetu, hapo kuna mapungufu makubwa.

Ni busara tukaangalia tunakoelelea, kabla ya kutoa majibu mepesi. Ni lazima tufikirishe akili zetu kwanza.

Naongea huku nikitanguliza maslahi mapana ya vijana wote wa Tanzania waliojiajiri kupitia utalii na biashara ya huduma (tourism and hospitality) nawapenda na kuwaheshimu mno, ila niwaambie uhalisia ulivyo, kuna mahali tulichelewa sana.

Hivi karibuni nilisoma kupitia blogu moja ya habari wakati nikiwa kwenye basi linalosafiri kuelekea mkoa mwingine. Nilikutana na habari ya kushangaza ikihoji: "nani mwenye hatimiliki na filamu ya Tanzania Royal Tour"? Nilicheka sana, hata kumbukumbu zikanivuta nyuma hadithi tajwa ya 'Sikuelewa ya Majaliwa.'

Nikajiuliza kama Watanzania tutaanza kuhangaika kwenye vitu vidogo kama mirabaha ya 'Tanzania Royal Tour', tutakuwa taifa mfu. Nani ambaye hakumbuki shida waliyopata wadau wa utalii katika kipindi cha UVIKO-19?

Ikajulikana, mamia ya wafanyakazi walipoteza ajira, nchi ilipoteza mapato, wafanyabiashara walipata hasara na sekta ya utalii iliyumba. Hiyo imenifikirisha sana kwamba kuna wanasiasa wanaopinga na hawana 'kesho yao'. Pia, ninaona kuwapo wabinafsi wasiopenda kuona taifa linasonga mbele kupitia utalii.

Nikamkumbuka Rais Paul Kagame, kimoyomoyo na uwekezaji wa utalii pale nchini kwake Rwanda, nikisema binafsi "ama kweli kwenye miti hapana wajenzi, kumejaa wakata mkaa watupu."

Rais Kagame mwaka 2018, baada ya kuingia mkataba na klabu ya soka ya Arsenal ya Uingereza kuhusu utalii wa Rwanda, aliona hiyo haitoshi, akaamua kuwekeza na klabu ya PSG ya Ufaransa kwa ajili kutangaza utaliiwa nchi yake.

Kwanini tutafute majibu mepesi kwa ajili ya utalii wetu? Lipo tatizo mahali kwa kipindi cha miaka mitano nyuma iliyopita, katika nchi yetu mahusiano ya kidiplomasia yaliyumba, tishio la Uviko - 19 lilipoteza nuru ya taifa hili kupitia utalii.

Kupitia Uwekezaji wa Rais Kagame kuutangaza utalii wa nchi yake, rafiki yangu mmoja aliwahi kuniuliza swali "hivi Rwanda kuna kivutio gani kikubwa cha kushawishi hadi waende kutangaza Rwanda, kwenye jezi ya klabu kubwa kama PSG, timu anayocheza Lionel Messi, mtu maarufu ulimwenguni? Wana vitu gani ambavyo Tanzania hatuna hadi waende kufanya promosheni kubwa kama hii?

Huenda maswali hayo ya namna hii yalikuwa kichwani kwa Rais Samia, kwa awamu hii ya sita ni faraja kwetu sisi Watanzania kuamua kutumia muda wake na nafasi ya kutangaza vivutio vya nchi. Hili si jambo la mchezo!

Rais ameona tukiendelea kufanya mchezo tutaachwa mbali bora atoke na kutangaza utalii wetu kuwavutia wawekezaji watu kama kina Rihanna, JayZ, Beyonce, David Beckham, Jeff Benzo na Ellon Musk, watu ambao wakija Tanzania, dunia itaangalia na itapata mvuto kuijua nchi ipo sehemu gani na kuzifahamu fursa zilizopo hapa.

Shughuli za utalii zinaendana sana na utamaduni, pamoja na sanaa yetu. Hivi vitu vimeshikana na ndiyo maana Rais Samia, amevibeba vyote kwa pamoja.

Kazi kwao kwa wadau wa utalii, sanaa na wasanii kushirikiana kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa. Alilolifanya Rais Samia, ni wazo linaloleta matokeo chanya.

Rais ametupatia promsheni ya kutosha tuboreshe huduma kwa wateja wetu na ziwe na viwango. Jukumu letu ni kulinda jina letu juu ya utalii husika.

Narudi tena kuuambia umma ukae kusikia, kila nchi ina vivutio vya vyake vya utalii na ina namna yake ya kutangaza vivutio na huduma za utalii iliyo nayo.

Tunaweza kujiuliza, nchi jirani ilipoanza kutumia jina la Mlima Kilimanjaro na kuutangaza kuwa ni mali yao, tatizo lilikuwa ni Rais Samia? Mtu atagundua jibu ni hapana na tulikuwa nyuma kwenye kuitangaza nchi yetu hasa kwenye utalii.

Rais anapofanya sinema ya 'Royal Tour' anabeba vitu vingi, vijana watapata ajira wanazozilia. 'Royal Tour' hiyo itakuza uchumi wa nchi kwa kuongeza watalii na hela za kigeni zitaongezeka na huduma za kijamii zitaongezeka.

Kama Watanzania na wadau wa utalii, tunapaswa kumuombea na kumtia nguvu Rais wetu kwa jitihada anazofanya juu ya kuinua taifa letu.

Tanzania, nchii yenye utitiri wa vivutio, hifadhi na mbuga za wanyama mbalimbali kushindwa kusonga mbele kiuchumi, haiwezekani hata kidogo! Madini yapo lakini yana ukomo, utalii upo leo kesho na hata milele. Niseme, Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni.

***• Kalamu ya Billal Saadat; Kazi Iendelee, Mama Yuko Kazini.***



Rais Samia Suluhu Hassan, katika mandhari tofauti ya sinema Royal Tour, inayotangaza utalii wa nchi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Kama Watanzania na wadau wa utalii, tunapaswa kumuombea na kumtia nguvu Rais wetu kwa jitihada anazofanya juu ya kuinua taifa letu.**





## UNESCO yawezesha sensa watu kidijitali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya watoto (UNICEF) limetoa vishkwambi 830 kwa serikali, kwa ajili ya utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi iliopangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Akizungumza jijini hapa, Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi na Spika wa Bunge Mstaafu, Anne Makinda, alisema hii ni mara ya kwanza Tanzania inaendesha shughuli hiyo kwa njia ya kidigitali ikiwemo matumizi ya vifaa vya kisasa.

"UNICEF wametuokoa. Unaweza usione umuhimu wa vishikwambi hivi lakini tunashukuru sana kwa sababu tumepanga kufanya sensa ya kidigitali ambayo haitatumia makaratasi," alisema Makinda.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema sensa ya mwaka huu itafanyika kidigitali kwa mara ya kwanza na haitotumia makaratasi hivyo itatumia vishikwambi katika kukusanya na kutunza taarifa.

Kutokana na hilo aliwapongeza wadau hao kwa kuiunga mkono serikali na kuwahamasisha wadau wengine kujitokeza kwa wingi kuungana na serikali ili kuhakikisha inafanyika kwa njia ya kisasa na ufanisi wa hali ya juu.

"Sensa inaenda kufanyika kidigitali ambayo haitatumia makaratasi. Matumizi ya vishikwambi ni muhimu kwa sababu yatarahisisha kazi ya ukusanyaji taarifa na kufanya Tanzania kuingia katika orodha ya nchi chache ambazo zinatumia teknolojia hiyo," alisema Dk. Chuwa

Naye Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Abdulmajid Jecha, alisema dunia sasa imebadilika kwa kuanza kufanya mambo yake kidigitali na Tanzania haina budi kubadilka ili kuelekea huko.

Alisema duniani kote ukusanyaji wa taarifa na takwimu za vitu mbalimbali zimeanza kufanyika kwa kutumia njia za kidigitali ikiwamo matumizi ya vishikwambi na wamefanikiwa

Mwakilishi wa UNICEF Tanzania, Dk. Shalini Bahunguna, aliipongeza serikali kwa dhamira yake ya kutekeleza sensa ya watu na makazi kidigitali ikiwemo kuwataka watanzania kuwa tayari kushiriki sensa hiyo.

Alisema sensa ni muhimu kwa taifa katika kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla.

# Watoto 495,156 kufikiwa kuchanjwa chanjo polio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATOTO 479,156 wenye umri chini ya miaka mitano kutoka katika halmashauri zote nane za mkoa wa Dodoma, wanatarajiwa kufikiwa kupatiwa chanjo ya matone ya ugonjwa wa kupooza (polio).

Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Dodoma, Francis Bujiku, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na kampeni ya chanjo hiyo kwa ngazi ya mkoa huku akibainisha kwamba mkoa umepokea dozi 551,029 za chanjo hiyo.

"Wilaya ya Bahi imetengewa dozi 65,022 na kuwafikia watoto 56,541, Chamwino imepelekewa dozi 93,696 na kuwafikia watoto 81,474 huku Chemba imepewa dozi 65,726 na imepanga kuwafikia watoto 57,153 wakati Dodoma Jiji imepewa dozi 88,832 za chanjo na kuwafikia watoto 77,245," alisema Bujiku.

Alisema Kondoa DC imepewa dozi 55,657 za chanjo na inatarajia kuwafikia watoto 48,397, Kondoa TC imepelekewa dozi 12,876 za chanjo na kuchanja watoto 11,196, Kongwa DC ina dozi 87,337 na watawafikia watoto 75,945 wakati Mpwapwa DC inatarajia kuwafikia watoto 71,205 huku ikipelekewa dozi za chanjo 81,886.

Mratibu huyo alisema tayari chanjo zimekwishasambazwa katika halmashauri zote na vituo vitakavyohusika na uhifadhi wa chanjo wakati wa utoaji wa chanjo.

Kwa mujibu wa Bujiku, Mkoa wa Dodoma umepanga kuwa na timu za uchanjaji 1,151 ambazo zitapita nyumba kwa nyumba kuanzia leo hadi Mei Mosi mwaka huu.

Aliomba wananchi wa mkoa wa Dodoma kushiriki katika kampeni hiyo muhimu kitaifa kwa ajili ya kuwakinga watoto wenye umri chini ya miaka mitano dhidi ya polio na kwamba lengo la kampeni ni kuongeza uelewa kwa wanajamii kuhusu faida za chanjo ya polio.

"Katika mkoa wa Dodoma kiwango cha utoaji wa chanjo mbalimbali kwa watoto chini ya miaka mitano mpaka sasa umefikia lengo la asilimia 102," alisema.



Baadhi ya wabunge wakilia baada ya kuona jeneza lenye mwili wa aliyekuwa mbunge wa viti maalumu Mkoa wa Rukwa, Irene Ndyamkama, lilipofikishwa viwanja vya Bunge kwa ajili ya wabunge kuaga Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndumbaro atoa msimamo kuhusu serikali Kulinda haki za binadamu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema serikali inao nia ya dhati ya kuendelea kuchukua hatua za kisera, kisheria na kiutawala kukuza na kulinda haki za binadamu.

Dk. Ndumbaro alisema hayo jana kwenye kikao cha 71 cha Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kilichofanyika kwa njia ya mtandao huku kwa mara ya kwanza lugha ya Kiswahili ikitumika sambamba na lugha zingine kama lugha ya kazi.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amelipa kipaumbele suala la kulinda na kukuza haki za binadamu na haki za watu katika utekelezaji wa shughuli za serikali yake.

Dk. Ndumbaro alisema janga la UVIKO-19 limeathiri haki za uchumi na za kijamii za wananchi na kuwa serikali imezingatia haki za binadamu na watu kwa upana wake wakati wa kuandaa mikakati ya kupambana na janga hilo.

Hata hivyo, alisema serikali ilipata Sh. trilioni 1.3 za ufadhili kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwaka 2021 ambazo zilitumika kununua dawa na maeneo ambayo yaliathirika zaidi na janga hilo kama vituo vya afya, shule, mabweni kuchimba visima vya maji na kuimarisha programu za kuinua uchumi kwa kuzingatia makundi maalum hususani vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Aidha, Dk. Ndumbaro alisema katika kutekeleza wajibu wa kukuza na kulinda haki za watu, serikali imekuwa ikiongozwa na misingi ya utawala wa sheria na utawala bora.

"Pia majadiliano na ushiriki wa wadau yamekuwa yakifanyika katika kukuza haki za kiraia na kisiasa. Katika kukuza uhuru wa maoni na haki ya kupata taarifa, tozo za kusajili runinga za mitandao na magazeti na runinga za mitandao zilizokuwa zimefungwa kwa ukiukwaji wa kanuni za utangazaji zilifunguliwa,"alisema.

Kuhusu haki ya kushiriki kwenye masuala ya kisiasa, Dk. Ndumbaro alisema Rais Samia amekuwa mstari wa mbele kujenga uhusiano mzuri na vyama vyote vya siasa vikiwamo vya upinzani.

Alisema Serikali ina heshimu misingi ya demokrasia na uhuru wa watu, hivyo kumekuwa na jitihada za makusudi za kukuza haki za kiraia na za kisiasa.

"Katika kuhakikisha watoto wa kike wanapata fursa za masomo, serikali ilipitisha Waraka wa Elimu Na. 2 wa Novemba 24, 2021 kuruhusu watoto walioachishwa masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya kupata mimba kurudi kwenye mfumo rasmi wa elimu baada ya kujifungua,"alisema.

Kuhusu matumizi ya kiswahili, DK. Ndumbaro alisema lugha ya Kiswahili imekuwa na mchango katika kuhakikisha nchi inakuwa na amani na utulivu, mazingira ambayo yanawezesha wananchi kuendelea kunufaika na haki zao za msingi.



# Waliokosa mikopo vyuo vikuu wakumbukwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa vyuo vikuu wanaoshindwa kuendelea na masomo kwa kushindwa kulipa ada kutokana na kukosa mikopo, wamepata neema baada ya mdau wa maendeleo wa mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela kuzindua mfuko maalumu wa kuwasaidia kutimiza ndoto zao.

Mwaselela alizindua juzi mfuko huo ujulikanao kwa jina la Ndele Mwaselela Education Scholarship na alianza kuwalipia ada wanafunzi sita wanaosoma katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mbeya (CUCoM).

Alisema aliamua kuwasaidia wanafunzi hao baada ya kupokea maombi maalumu kutoka kwa viongozi wa chuo hicho kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaoacha masomo kutokana na kushindwa kulipa ada baada ya kukosa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Mwaselela ambaye ni mmiliki wa Shule za Patrick Mission ya Dar es Salaam na Paradise Mission ya Mbeya, alisema atatumia sehemu ya mapato yake kuwasomesha wanafunzi hao ili kufanikisha ndoto zao.

Alisema lengo lake ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha vijana wanasoma na kwamba mbali na wanafunzi wa vyuo vikuu pia amekuwa akisaidia wanafunzi wa ngazi zingine za chini.

"Nimeamua kuanza na wanafunzi hawa sita baada ya kujiridhisha kwamba uongozi wa chuo hiki umetumia mifumo sahihi ya kuwapata. Kwa leo (juzi) naanza kwa kulipa Sh. milioni sita na Julai nitalipa tena zingine ili watoto hawa wasome vizuri," alisema Mwaselela.

Alisema kabla ya kuanza kuwasomesha wanafunzi hao, alikuwa ameshasomesha wanafuni wengine zaidi ya 500 katika ngazi mbalimbali wakiwamo 15 katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Mkuu wa CUCoM, Prof. Romuald Haule, alisema waliamua kumwomba mdau huyo kuwasaidia kutokana na kuelemewa na wanafunzi waliokuwa wanaacha masomo kwa sababu ya kukosa ada.

Alisema baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakilazimika kuacha chuo kabisa na wengine walikuwa wanaahirisha miaka ya masomo ili wakatafute ada jambo ambalo alisema limekuwa kero kwa wanafunzi hao pamoja na uongozi wa chuo.

Alisema kutokana na kero hiyo watumishi wa chuo waliamua kutumia fedha zao kwa kuchangishana ili kuwalipia ada wanafunzi ambao walikuwa wako hatarini kuacha masomo na baada ya idadi kuongezeka, waliamua kuanza kutafuta wadau.

"Kwa mwaka huu pekee, zaidi ya wanafunzi 40 wameomba kuahirisha mwaka kwa sababu walikosa mikopo na hawana ndugu wenye uwezo wa kuwasaidia kulipa. Kwa hiyo tunashukuru kwa kukubali ombi letu," alisema Prof. Haule. Mkuu wa CUCoM, Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, alimshukuru Mwaselela kwa kuanzisha mfuko huo kuwa kwa sasa tatizo la wanafunzi kukosa mikopo limekuwa kubwa nchini.

Aliwaomba wadau wengine kusaidia wanafunzi hao kwa madai kuwa wanafunzi wengi wamekuwa wakifaulu vizuri na kuchaguliwa kujiunga na vyuo lakini wanaacha kwa sababu ya kukosa ada.



Mdau wa Maendeleo wa Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela (katikati), akionyesha hundi yenye thamani ya Sh. milioni sita ambayo aliukabidhi uongozi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mbeya (CUCoM) kwa ajili ya ada za wanafunzi sita waliokosa mkopo. Kushoto ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine (SAUT), Prof. Costa Mahalu na kulia ni Askofu Mkuu wa Kanisa katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Watakiwa kuandika habari kuhusu jamii

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewataka wandishi wa habari kuandika habari za kuisaidia jamii kiafya ikiwamo kuacha kutumia bidhaa ambazo zina madhara vikiwamo vipodozi na bidhaa za tumbaku.

Homera alitoa ushauri huo jana jijini hapa alipokuwa anafungua kikao kazi cha Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari ambacho kinafanyika kwa siku mbili.

Alisema wandishi wa habari wana jukumu kubwa la kuandika habari za kuwaelimisha wananchi ili waachane na matumizi ya bidhaa hizo badala ya kuandika habari baada ya madhara ya bidhaa hizo kutokea kwa wananchi.

Homera alisema vyombo vya habari nchini vina msaada mkubwa kwenye jamii endapo vitatumika vizuri lakini vikitumika vibaya, vinaiharibu jamii.

"Nawashukuru sana TMDA kwa kuamua kutoa mafunzo haya kwa wandishi wa habari na wahariri. Naamini mafunzo haya yatasaidia kuwaimarisha waAndishi hawa ili waandike vizuri zaidi," alisema Homera.

Aliwataka wandishi wa habari na wahariri wanaoshiriki mafunzo hayo kusikiliza kwa makini elimu inayotolewa ili wapate ujuzi utakaowasaidia kuandika habari hizo kwa usahihi.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, alisema katika mafunzo hayo waliwaalika wahariri wa vyombo vya habari vya mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Njombe pamoja na wahariri kutoka mkoani Dar es Salaam.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wandishi wa habari kuandika habari zinazohusiana na taasisi hiyo. Mbali na mafunzo hayo, alisema wako wandishi wa habari ambao watapatiwa vyeti vya uandishi bora wa habari zinazohusiana na taasisi hiyo.

# Wananchi walia kupanda kwa bei za bidhaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wananchi mkoani Mbeya wamelalamikia ongezeko la bei za bidhaa mbalimbali zikiwamo zile ambazo bidhaa hazikustahili kutokana na kuzalishwa ndani ya nchi na hazina uhusiano na kupanda kwa bei ya mafuta.

Wananchi hao walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya kukagua ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Kata ya Iziwa jijini Mbeya ambayo inajengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 600.

Kwa mujibu wa wananchi hao, kwa sasa hata mboga za majani ambazo zinazalishwa na wakulima wa kawaida, zimepanda bei hali ambayo walisema imeanza kuwakatisha tamaa.

Mmoja wa wananchi hao, Elia Tuyagaje, alisema kupanda kwa bei hizo kumesababisha hali ya maisha kuwa ngumu tofauti na ilivyokuwa miezi michache iliyopita, hivyo akaiomba serikali iwasaidie kudhibiti hali hiyo.

Alisema kwa sasa vifaa vya ujenzi bei yake ni kubwa na imesababisha baadhi ya watu kusimama ujenzi huku akiainisha vifaa ambavyo bei imepanda zaidi kuwa ni nondo na saruji.

"Tuachane na bei ya bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambazo tunasema zinasababisha na vita vya Ukrine na Russia lakini sasa mpaka mboga tunazolima wenyewe zimepanda. Mchicha tunalima wenyewe lakini bei juu," alisema Tuyagaje.

Naye Subira Mwalongo alisema bei ya unga wa nganio ambao hutumika kutengenezea maandazi na mafuta ya kupikia zimepanda kuliko kawaida hali ambayo inawafanya wapandishe bei ya chakula wanachopika tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema awali mfuko wa unga huo wenye uzito wa kilo 50, walikuwa wananunua kati ya Sh. 25,000 na 30,000 lakini kwa sasa wananunua Sh. 48,000 mpaka 50,000 huku bei ya mafuta ya kupikia ikiwa imefikia Sh. 140,000 kwa ndoo ya lita 20.

Alisema kutokana na tatizo hilo la kupanda kwa bei ya bidhaa baadhi ya wananchi watashindwa kumudu gharama za maisha na wengine watashuka kiuchumi.

"Uchumi wetu umekuwa mgumu sana kipindi hiki na visingizio vimekuwa vingi. Hatuelewi uhusiano uliopo kati ya kupanda kwa bei ya mafuta yanayotoka nje ya nchi na maisha yetu ya kawaida. Tunakuomba Mkuu wa Mkoa mtusaidie kushughulikia hili," alisema Mwalongo.

Akijibu malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema wa sasa wanatekeleza maagizo ya Waziri Mkuu ya kutembelea masoko ya mazao mbalimbali ili kujua uhalisia wa bei ya bidhaa.

Alisema halmashauri zote za mkoa zinaendelea kuwasilisha taarifa za hali ya bei ya bidhaa kwa mkuu wa mkoa na kwamba baada ya kazi hiyo, wataanza kushughulikia wanaopandisha bei holela.

Dk. Chuachua aisema serikali itawachukulia hatua wafanyabiashara wote watakaobainika kuwa wanapandisha bei ya bidhaa bila kufuata utaratibu.



# Bil. 67/- kuimarisha afya, elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, ameliomba Baraza la Wawakilishi kuidhinisha Sh. 67,368,924,250 kwa ajili ya matumizi ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Hemed alitoa rai hiyo jana wakati akisoma hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema afisi yake kwa mwaka wa fedha 2022/23 imepangiwa kukusanya Sh. 92,826,495.

Katika hotuba hiyo alisema mipango ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha ni kuboresha sekta mbalimbali zikiwamo afya, alimu, maji safi na salama na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi, Hemed alisema serikali imeshaanzisha Wakala wa Uezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar na hatua hiyo itasababisha uratibu mzuri na wa uhakika katika kutekeleza azma hiyo.

"Bila shaka uanzishwaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar kuwezesha pamoja na mambo mengine masuala ya mafunzo na upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa wajasiriamali na wafanyabiashara pamoja na upatikanaji wa masoko kwa bidhaa wanazozalisha au huduma wanazotoa," alisema.

Pia aisema Serikali ya Zanzibar inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kutekeleza malengo iliyojowekea na kuwashukuru wadau hao katika kuunga mkono shughuli za maendeleo nchini.

Hemed alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa mashirika ya kitaifa na kimataifa ili yaendelee kufanya kazi kwa usalama na amani.

Aliwataka wafanyabishara kuendelea kuuza bidhaa zao kwa bei nafuu kama zilivyoelekezwa na mamlaka za serikali ili kuwapa nafuu wananchi hasa katika kipindi hiki na kuzingatia ukusanyaji wa mapato pamoja na faida kwa wafanyabiashara.

Hata hivyo, alisema kupungua kwa maradhi ya UVICO - 19 duniani, Zanzibar imekuwa na mabadiliko ya kiuchumi kutokana na kuimarika zaidi kwa sekta za huduma.

Alisema baada ya kupunguza kwa maradhi hayo, sekta za huduma zimeimarika na kufikia wastani wa asimilia 6.8 kutoka asilimia 1.0.

Pia alisema mabadiliko ya ukuaji wa sekta za huduma yalitokana na kuimarika kwa shughuli za utalii, kuimarika kwa sekta ya fedha kufikia asilimia 9.9 kutoka asilimia 2.1.

Alibainisha kwamba kufuatia kuimarika kwa shughuli za uwekezaji pia kulipelekea kuongezeka kwa Shughuli za ujenzi na kufikia asilimia 8.9 kutoka asilimia 6.5 ambapo sekta ya umeme na gesi kufikia asilimia 8.0 kutoka asilimia 2.8.

Akizungumzia kuhusu uchumi wa Zanzibar, alisema umeimarika na kufikia asilimia 5.1 mwaka 2010 na mwaka 2022 unatarajia kufikia wastani wa asilimia 6.8.

## Maeneo 148 yaathiriwa na tabianchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema maeneo 148 ywa Unguja na Pemba yameathiriwa na mabadiliko yqa tabianchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, aliyasema hayo wakati akijibu suali la la Mwakilishi wa Gando, Maryam Thani Juma, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mwakilishi huyo alitaka kujua maeneo mangapi yameathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi kwa Zanzibar.

Waziri Harusi alisema kwa Unguja ni maeneo 123 na Pemba ni 25 na kati ya hayo, yamo ambayo yameshaanza kuchukuliwa hatua mbalimbali na yale ambayo yanategemewa kuchukuliwa hatua baada ya kipindi cha bajeti.

Naye Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, alitaka kujua katika kisiwa cha Kojani katika eneo la Kivuko, kuna mbuyu ambao ni hatarishi na bado hakuna hatua hazijachukuliwa, hivyo jambo hilo limefika wapi.

Waziri Harusi alisema mbuyu ulioko Likoni Kojani wameshaenda kuukagua na kuuona kweli unastahili kushughulikiwa.

Alisema katika ushughulikiaji wa mbuyu huo haujitaji kuondoshwa bali unahitaji kujengewa mazingira mazuri ili kuendelea kulinda mazingira ya bahari katika eneo la Kojani.

Harusi alimthibitishia mwakilishi huyo kuwa wizara yake iko katika hatua za mwisho kujenga ukuta wenye ukubwa wa mita 100 kwa lengo la kuihifadhi ufukwe huo na si kwa mbuyu pekee.

Miraji Khamis Mussa kutoka Jimbo la Chumbuni, aliipongeza serikali kwa maeneo ambayo yalikuwa yanaleta mazingira mabaya yakiwemo Kiembesamaki, Mbweni, Mwanakwerekwe na Shaurimoyo kwa ujenzi wa mitaro ya michirizi kwa ajili ya kuondoa maji na kupeleka pwani.

Hata hivyo, alitaka kujua kuna utafiti gani wa kimazingira uliosababisha kufanya jambo hilo na baadaye kuonesha athari ambazo ardhi itakuwa kavu na ardhi kukosa maji kabisa.

Waziri Harous alisema serikali kabla ya kufanya jambo lolote kwanza hufanya utafiti wa kina hivyo katika kuondosha maji katika maeneo hayo utafiti wa kutosha umefanyika na kuona kwamba yaliyoondoshwa na yatakayobaki hayatoendelea kuathiri shughuli za maendeleo ya wananchi.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Rehmat-Fi-Sabililah Trust of Zanzibar, Hajat Yasmin Alloo, akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watoto baada ya kukabidhi hati maalumu na zawadi mbalimbali kwa watoto 1,220 wa Unguja na Pemba, waliofunga Swaumu, kusoma Quran tukufu, Darsa na kusali Taraweh katika mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani jana. Aliyekaa kwenye kiti ni Zehra Esmail Alloo (96) mmoja wa wanzilshi wa mfuko huo. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## TMA yatoa tahadhari kuhusu masika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imewataka wananchi kuchukua tahadhari hasa katika kipindi hiki cha mvua za masika zinazoendelea kunyesha ili kuepukana na majanga ambayo yanaepukika.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Mamalka hiyo Ofisi ya Zanzibar, Muhammed Vuai, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya miaka 58 ya Muungano katika viwanja vya Maisara, mjini Zanzibar.

Aliwata wananchi kufuatilia utabiri wa hali ya hamlaka hewa unaotolewa na mamlaka hiyo ili kuwa na taarifa za uhakika kuhusu hali ya hewa.

Vuai alisema tahadhari inatakiwa ichukuliwe na mifumo ya hali ya hewa inapoashiria kuwepo kwa mvua mamlaka hiyo hutoa tahadhari mapema ili kulinda maisha ya watu na mali zao.

Alisema wanadhibiti taarifa zote za hali ya hewa na inatoa huduma katika taasisi mbalimbali zikiwamo usafiri wa anga, baharini, masuala ya kilimo, madini na utalii.

"Huduma za hali ya hewa ni mtambuka katika kuhakikisha wanaokoa maisha ya watu na kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Vuai pia alisema mabadiliko ya tabianchi yameathiri mabadiliko ya hali ya hewa ndiyo maana wakati mwingine hutoa utabiri lakini kukawa na matokeo tofauti.

Aidha, aliwataka wananchi kufika katika maonyesho hayo ili kujifunza na kupata taarifa mbalimbali za mamlaka ya hali ya hewa.

Akitembelea maonyesho hayo, Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Awadhi Haji Juma, alisema yamefana kutokana na kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama.

"Jeshi la Polisi litahkikisha linaimarisha ulinzi na usalama muda wote, hivyo wananchi wasiwe na hofu, waendelee na shughuli zao hasa katika kipindi hiki tunachoelekea cha Skukuu ya Iddi el Fitr," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamiziwa mirathi Na 17/2007**

**Harid Swadiko Mwasumilwe.....Marehemu**
**Zena Harid Mwasumilwe......Msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI.**

Watu wote wanaodai kuwa na haki na marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 14 ya mwezi mei mwaka 2022.

Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 14 aprili mwaka 2022.

Hakimu Mkazi

---

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA BABATI
MKOA WA MANYARA
MAOMBI NA.71/2020
SERAPHINE RICHARD.......MLETA MAOMBI.
DHIDI YA
ERICK MMARI......MJIBU MAOMBI
**Mdai popote ulipo.**

Fahamu kwamba mleta Maombi SERAPHINE RICHARD ameleta Maombi Na. 71)2020 dhidi yako.
Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi,wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria,Shauri limepangwa kutajwa tarehe 27/4/2022.
Endapo hautatekeleza hayo Shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
Endapo hautatekeleza hayo Shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 21/3/2022.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) BABATI**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya CHAMWINO MJINI
Wilaya ya DODOMA MJINI
Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA
Usimamizi wa mirathi Na 49/2022
Jina la Mdai:ENJO TUMAIN
Jina la Mdaiwa JEREMIA MAZENGO
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa JEREMIA MAZENGOWA BIHAWANA K.K
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba (Eleza hapa habari za Madai) VYOMBO
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii ALHAMISI tarehe 3 Mwezi 05 Mwaka 2022 Saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila yaw ewe kuwepo
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi 04 Mwaka 2022

.............. ..............
**HAKIMU**

---

## TANGAZO LA NOTISI WADAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITE**D, Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) Kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa kwa wadaiwa watakaoshindwa kulipa madeni yao ndani ya muda ulioainishwa( siku sitini).Ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kuuza mali zao ambazo zimetumika kama dhamana za mikopo yao.

**Wadiwa Sugu ni: -**
Revocatus Lucas Suzuguye –Kitunda (DSM)
Simon Francis Mziray – Sigara Buza (DSM)
Khadija Hussein Safarah- Mgeninani (DSM)
Omary Bakari Wachopa -Churwa (Mkuranga)
Gregory Isdory Wenceslaus – Kimara (DSM)
Jemsi Paul Kitonga –Kurutini (DSM)
Hamida Mohamed Alley – Tandika (DSM)
Ally Amir Kasongo - Chamanzi (DSM)
Mussa James Kazundu –Chanika - Mgeule (DSM)

**Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AUDACIA INVESTMENT LTD** inatangaza Kupotea kwa kadi ya gari aina ya **RANGE ROVER EVOQUE** yenye namba za ujasili **T 111 DEN,** CHASIS NO. **SALVAZAE0FH042308,** ENGINE NAMBA **DZ884042946224DT.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**KW/RB/2070/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MIRATHI NAMBA: 35....2021**

**MUOMBAJI: TELESIA JOSEPH**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: ROBERT JOSEPH**

**Kwa: ROBERT JOSEPH**

**Ombi la mdai: TELESIA JOSEPH**
**Madai ya : MIRATHI**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 28 mwezi 04 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 10/04/2022.

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIUS BYABATO NDYAMUKAMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.119/57** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari KIBAHA mwaka 1974 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0134/0607** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari MOSHI mwaka 1976. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/163315**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALLEN JULIUS MGENI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1080/0110** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari MUHEZA MUSLIM mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA: **MUH/RB/969/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELICK BICHAMAKALA DAVID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1028/0032** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BUTUNDWE SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: KIL/MOS/RB/157278/2022.**

---

TEGEMEZA FINANCE COMPANY AND COURT BROKER
P.O. Box 77593 – DAR ES SALAAM.

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa mamlaka tuliyopewa na Mahakama Kuu kitengo cha Kazi, tunarudia kutangaza uwepo wa mnada wa hadhara.

Kesi namba 578/2022
Mdai Michael Mkwela & 2 others.
Mdaiwa Mikocheni Resort Centre.

| Mali itakayouzwa | Tarehe ya Mnada | Eneo mnada utakapofanyika |
|---|---|---|
| Gari namba T 198 DLT aina ya IST | 29/4/2022 | Mbezi Beach Bondeni Saa 4 asubuhi. |

Taratibu za mnada kuzingatiwa.

**Kwa mawasiliano Zaidi piga simu namba 0719 187 677**
**WATU WOTE MNAKARIBISHWA.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **JOSEPH LAURENT ANTHONY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUBARU lenye namba za usajili **T382DRE**, injini namba **EL15D673814** na chassis namba **GH2025210.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/163883/2022**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi au apige simu namba **0711265777.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Waumini wa Kikristo wa madhehebu ya Orthodox wakishiriki ibada mbele ya kanisa takatifu la Virgin mjini Kyiv, ambalo limeathiriwa na mashambulizi ya Russia yanayoendelea nchini Ukraine. **PICHA: REUTERS**

# Russia yazuia gesi kwenda Poland, Bulgaria, yadai kushikilia miji mingine minne Ukraine

**LONDON,** UINGEREZA

KAMPUNI ya nishati ya Russia, Gazprom imetoa taarifa kwa nchi za Poland na Bulgaria kuwa inasitisha kuzisambazia nishati ya gesi kuanzia jana.

Taarifa kutoka kampuni ya gesi ya Poland (PGNiG) ilisema iliambiwa itasimamishiwa usambazaji wa gesi kuanzia saa mbili za asubuhi ya jana, sawa na saa 12 alfajiri kwa Afrika mashariki.

Wizara ya nishati ya Bulgaria, pia ilisema ilifahamishwa kwamba usambazaji wa gesi utasitishwa kuanzia Jumanne.

Hatua hiyo imechukuliwa na Russia baada ya kutoa onyo kwa nchi zisizo rafiki lazima zianze kulipia gesi kwa sarafu ya rouble, vinginevyo itasimamisha usambazaji.

### NCHI ZOTE MBILI ZIMEKATAA KULIPA KWA NJIA HIYO.

PGNiG hutegemea kampuni ya Gazprom kwa sehemu kubwa ya gesi yake inayoagizwa kutoka nje na ilinunua asilia 53 ya mafuta yake kutoka Russia katika robo ya kwanza ya mwana huu.

Ilielezea usitishwaji huo wa usambazaji wa gesi kama ukiukaji wa mkataba, na kuongeza kuwa kampuni itachukua hatua kurejesha upatikanaji tena wa nishati hiyo. Bulgaria, ambayo hutegemea kampuni Gazprom kwa zaidi ya asilimia 90 ya gesi yake, ilisema imechukua hatua za kutafuta vyanzo mbadala.

Wizara ya nishati ya nchi hiyo alisema kuwa Bulgaria ilitekeleza majukumu yake chini ya mkataba na Gazprom kwa kufanya malipo yote yanayohitajika.

Iliongeza kuwa mfumo mpya wa malipo uliopendekezwa na Russia ni uvunjaji wa mkataba uliopo.

Kufuatia taarifa hizo, wizara ya hali ya hewa ya Poland ilisema kuwa usambazaji wa nishati nchini humo uko salama.

Waziri Anna Moskwa, alisema kuwa hakuna haja ya kuchukua gesi kutoka kwenye akiba itakuwa ni kuipunguza.

Naibu Waziri wa mambo ya nje wa Poland, Marcin Przydacz, alisema nchi yake imekuwa ikijiandaa kwa uwezekano wa Russia kupunguza mauzo ya gesi kwa kutafuta wasambazaji wengine wa gesi.

"Nina uhakika kwamba tutaweza kulishugulikia hili ," aliiambia BBC.

Aliongeza kuwa kusitishwa kwa usambazaji wa gesi kunaonyesha kuwa sio mshirika wa kuaminika katika aina yoyote ya biashara na akazitaka nchi nyingine za Ulaya kama Ujerumani kuunga mkono marufuku ya kuagiza nishati kutoka Russia.

Poland tayari ilikuwa inajiandaa kusitisha uagizaji wa gesi kutoka Russia ifikapo mwishoni mwa mwaka, wakati mkataba wake wa muda mrefu na Gazprom utakapomalizika.

PGNiG ilisema akiba yake ya gesi iliyopo chini ya ardhi imejaa kwa takriban asilimia 80 na wakati kipindi cha majira ya joto kinakaribia, gesi itakayohitajika itakuwa ya kiwango cha chini.

Poland pia ina vyanzo mbadala vya usambazaji wa gesi inayotumia, ukiwemo mfumo wa gesi asilia (LNG) katika eneo la Swinoujscie.

Mei mosi bomba jipya gesi linalounganisha na Lithuania pia litazinduliwa ambalo litaipatia Poland uwezo wa kupata gesi kutoka bomba la Lithuania la LNG.

Bomba lingine jipya linalosambaza gesi kutoka Norway, linalofahamika kama the "Baltic Pipe", litaanza kutumiwa katika mwezi Oktoba.

Linatarajiwa kuwa na uwezo kamili kufikia mwishoni mwa mwaka na linaweza kuchukua nafasi ya mauzo ya gesi kutoka Urusi.

### RUSSIA YADAI KUTEKA MIJI MINGINE

Kulingana na shirika la habari la Interfax la Russia, wanajeshi wake wamefanikiwa kupata udhibiti kamili wa eneo lote la mkoa wa Kherson, pamoja na sehemu za miji ya Kharkiv, Zaporizhzhia na Mykolaiv.

Katika hotuba yake kwa taifa juzi, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alikiri Warusi walikuwa wakijaribu kuweka nguvu ya udhibiti katika eneo lililotekwa.

"Waliendelea kushambulia askari wetu karibu na Kharkiv, huko Donbas," alisema.

"Wanajaribu kuonyesha madai ya serikali mpya huko Kherson na sehemu ya eneo la Zaporizhzhia." aliongeza

Kituo cha utawala cha kikanda cha Kherson, jiji la Kherson, kilitekwa katika siku za mwanzo za vita. Lakini Pentagon baadaye ilisema wanajeshi wa Russia walikuwa wamepoteza udhibiti wake. Kherson ndio eneo lenye idadi kubwa zaidi ya watu inayoshikiliwa na Urusi hadi sasa.

Rais Putin alidai juzi kwamba mapigano huko Mariupol yamemalizika. Mji huo wa kimkakati wa bandari ya kusini umekumbwa na mashambulizi ya Urusi ambayo yaliwaacha wapiganaji wapatao 1,000 wa Ukraine wakiwa wamezingirwa.

### MATAIFA YA ULAYA KUPELEKA NDEGE VITA

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza Liz Truss, alisema Uingereza na mataifa mengine yenye nguvu ya Magharibi yanapaswa kutoa ndege za kivita kwa Ukraine kama sehemu ya msaada wao wa kijeshi wa muda mrefu.

Katika hotuba yake aliyoitoa mjini London, alisema nchi za Magharibi zinapaswa kuwa tayari kutoa msaada kwa nchi hiyo.

Ukraine imeomba mara nyingi ndege za kivita, hasa zilizotumika zama za Usovieti ambazo marubani wao wanazifahamu.

Washirika wa nchi za Magharibi wamesita kufika hatua hiyo kwa hofu ya kuichokoza Urusi.

Lakini wakati wanachama wa Nato wakiongeza uungaji mkono wao kwa Ukraine kwa silaha za masafa marefu, Truss alisema wanapaswa kwenda mbali zaidi.

bgtl

**BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapo chini, walipe madeni wanayodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mikopo yao kwa **MNADA WA HADHARA**.Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAWI |
|---|---|---|---|
| 1. | ABILAH HASSAN MATENDE | Nyumba Ya Makazi Yenye Hati Ya Mauziano Iliyopo Majohe Rada karibu na msikiti wa Shehe Juma Manispaa Ya Ilala | ILALA |
| 2 | ERASMI MATHIAS SHIRIMA | Nyumba Ya Makazi Yenye Hati Ya Mauziano Iliyopo Boko Dovya Mtaa Wa Burumawe Changamoto | KINONDONI |
| 3 | IBRAHIMU ELIUDI MANOSHA | Nyumba ya makaziyenye hati ya mauziano iliyopo Vikawe Shina Bondeni | KINONDONI |
| 4 | ILAMBONA LUGE HWAGO | Nyumba Ya Makazi yenye kiwanja namba 651,kitalu "A" Iliyopo Kunduchi Mtongani wilaya ya Kinondoni Hati namba 96246 L.O 410818 Kwa Jina La Deusdedith Alphance Mitanto. | KINONDONI |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**
**Email: info@bestgoup.co.tz**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

# ATUPELE NJE BIASHARA IKIWAVAA MBEYA CITY

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo kwa wenyejji Mbeya City kuwakaribisha Biashara United kutoka Musoma kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Biashara United, Frank Wabare alisema timu yake itawakosa wachezaji wanne kutokana na sababu mbalimbali na aliwataja nyota hao watakaokosekana ni Atupele Green, Deo Mafie, Salum Kipaga na Ibrahim Ndunguli.

"Ingawa tutawakosa wachezaji hao wanne, haitatuathiri kwa sababu tulisajili wachezaji wengi wenye uwezo wa kupambana na kuisaidia timu," alisema Wabare.

Kiongozi huyo alisema mikakati yao ni kupata pointi tatu muhimu kutoka katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani.

"Morali ya kila mchezaji ipo vizuri kuhakikisha tunapata matokeo ingawa tumekaa muda mrefu bila kucheza, mara ya mwisho tulicheza ilikuwa April 6," Wabare alisema.

Aliongeza wamejiandaa kuhakikisha wanapata matokeo chanya ili wapande hadi katika nafasi salama kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

"Tunataka kujiimarisha katika msimamo, lengo letu ni kumaliza kwenye nafasi za juu na kujihakikisha kuendelea kushiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara msimu ujao," aliongeza Wabare.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule alisema wamejiandaa vizuri kubakiza pointi tatu nyumbani ili kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

Wakati Lule akusema hayo naye Kocha wa Biashara United, Vivier Bahati alisema wamejipanga kuleta ushindani katika mchezo huo kwa kutafuta pointi muhimu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya msimamo wa ligi.

"Biashara United ni timu nzuri, tuko nyumbani tutacheza kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu kwa sababu ya kila moja tunahitaji pointi ili kufikia malengo yao ikiwemo kwetu tunahitaji kupambana tumalize msimu katika nafasi nne za juu ili msimu ujao tukashiriki Kimataifa," alisema Lule.

Vivier alisema: "Ligi imekuwa ngumu, tuna waheshimu Mbeya City tutacheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu tunafuta pointi muhimu ili kufikia malengo yetu ya mwisho wa msimu tunakuwa miongoni mwa timu zitakazoshiri ligi."

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Geita Gold FC kuwavaa Azam FC kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu uliopo mkoani Geita.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo (kushoto), akimkabidhi kiungo wa zamani wa Simba na Yanga, Athumani Iddi (kulia), cheti cha Ukocha ngazi ya CAF Diploma D baada ya kuhitimu kozi hiyo hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Coastal yaipania Polisi Tanzania

**Na Cheji Bakari,** TANGA

BAADA ya kuendelea kupoteza mechi ugenini, kikosi cha Coastal Union kimeendelea kujiimarisha ili kusaka ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania itakayochezwa Mei 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga.

Msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi aliliambia gazeti hili wanatarajia kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ili kurejesha matumaini ya kutoshuka daraja.

Wandi alisema benchi la ufundi limeendelea kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi zilizopita na imani yao ni kuona wanautumia vyema uwanja wa nyumbani.

"Katika mechi ijayo dhidi ya Polisi Tanzania tutapambana kwa nguvu zote, tunatarajia kutimiza malengo ya kuvuna pointi tatu, lakini kama itatokea mengine basi ndio matokeo ya mchezo," alisema Wandi.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, Coastal Union yenye pointi 21 iko katika nafasi ya 14 ikifuatiwa na 'Maafande' wa Tanzania Prisons yenye alama 19 na Mbeya Kwanza FC yenye alama 18 inaburuza mkia kwenye ligi hiyo.

Tangu Juma Mgunda arejee katika benchi ya ufundi, timu hiyo imepoteza michezo yote iliyocheza dhidi ya mabingwa watetezi, Simba, Tanzania Prisons FC na Mbeya Kwanza.

# Makapu akalia kuti kavu Polisi

**Na Shufaa Lyimo**

KAMATI ya Utendaji ya Polisi Tanzania inatarajia kukutana hivi karibuni kwa ajili ya kujadili hatima ya mchezaji wao, Said Makapu ambaye alitoroka kambini kwa madai ya kukasirika kutopangwa katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Polisi Tanzania, Michael Mtebene alisema tayari mchezaji huyo amerejea kambini lakini hakusafiri na kikosi cha timu hiyo kuelekea Mbeya mpaka tatizo lake la utovu wa nidhamu litakapotolewa uamuzi.

"Makapu yupo kambini, amerudi tangu April 22, mwaka huu na uongozi haujazungumza naye chochote mpaka hapo kamati itakapokutana, hawezi kuruhusiwa kusafiri wakati amekiuka kanuni na taratibu za mkataba," alisema Mtebene.

Katibu huyo alisema Makapu atachukuliwa hatua na lengo la kufanya hivyo ni kutoa fundisho kwa wengine wasifanye kosa la aina hiyo.

"Kamati itakutana na tutampa Makapu nafasi ya kujieleza kwa kumsikiliza halafu tutatoa uamuzi kwa kuzingatia taratibu za kinidhamu," Mtebene alisema.

Aliongeza mshambuliaji, Adam adam atakuwa sehemu ya kikosi kitakachoikabili Tanzania Prisons katika mechi itakayochezwa Mei Mosi, mwaka huu baada ya kumaliza adhabu yake.

Naye Mwenyekiti wa timu hiyo, Charles Mkumbo, alisema Makapu amefanya makosa hivyo lazima atawajibishwa.

Mkumbo alisema suala la kupangwa au kutopangwa katika mechi yoyote lipo chini ya mwalimu, hivyo kufanya jambo ambalo halistahili ni makosa.

"Lazima awajibishwe kisheria tunatakiwa tumpe adhabu ambayo hawezi kurudia kufanya hivyo kwa mara nyingine hawezi kuishi anavyotaka yeye,alisema Mkumbo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**PSG, MBAPPE KITAELEWEKA**

KLABU ya Paris St-Germain ina matumaini mshambuliaji wake, Kylian Mbappe, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid, atasaini mkataba mpya baada ya mazungumzo yao na mama wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 wiki iliyopita. (*Telegraph*)

**TCHOUAMENI ATAKIWA**

LIVERPOOL imefanya mawasiliano na kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22. (Foot Mercato)

**UNITED, DE GEA KUTETA**

KLABU ya Manchester United inapanga kuzungumza na golikipa wa Hispania, David de Gea mwenye umri wa miaka 31 kuhusu mkataba mpya. (*90 Min*)

**HALLER ANUKIA UNITED**

MANCHESTER United huenda ikaangukia pia kwa nyota wa kimataifa wa Ivory Coast, Sebastien Haller mwenye umri wa miaka 27. Mshambuliaji huyo kwa sasa anacheza chini ya kocha ajaye wa United, Erik ten Hag pale Ajax. (Sun)

**DE BEEK MAMBO SAFI**

KIUNGO Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 25, atapewa nafasi Manchester United msimu ujao na kocha Erik ten Hag. (*Telegraph*)

**ASRNEAL YAMTAKA ABRAHAM**

ARSENAL watahitaji kutoa kitita cha pauni milioni 67.7 ili kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 24 kutoka AS Roma. (*Football London*)

**KOUNDE NJIA MOJA**

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Jules Kounde anataka kuondoka Sevilla msimu wa joto na nyota huyo mwenye miaka 23 anaitazama kujiunga na Chelsea. (*Times*)

**PIEPER KUTUA CHELSEA**

CHELSEA inamfuatilia mlinzi wa Ujerumani, Amos Pieper mwenye umri wa miaka 24, ambaye mkataba wake na Arminia Bielefeld unamalizika mwishoni mwa msimu. (*Mirror*)

**HOJBJERG AKARIBIA SPURS**

NEWCASTLE inamtaka kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 26. (*Express*)


**LEWANDOWSKI NI BARCA**

KUNA matumaini makubwa pale Barcelona ikampata mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33 akitokea Bayern Munich. (*Sport*)

**MODRIC KUPEWA MKATABA**

NYOTA wa kimataifa wa Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 36 anajiandaa kusaini mkataba mwingine mpya Real Madrid utakaomalizika mwakani. (*Fabrizio Romano*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AFUNGUKA CITY INA KAZI KUBWA

### Ni kutokana na kiwango ilichokionyesha katika mchezo wao dhidi...

**MANCHESTER,** ENGLAND

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema bila umakini mkubwa ndani ya dakika 90 kwa timu yake katika mchezo wa pili, hatawaweza kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya ushindi wao wa mabao 4-3 dhidi ya Real Madrid, hapo juzi.

City walianza kwa kasi katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza Jumanne, mabao ya Kevin de Bruyne na Gabriel Jesus yakiwaweka mbele kwa 2-0 ndani ya dakika 11. Kulikuwa na hisia inaweza kuwa zaidi, lakini kila wakati kikosi cha Guardiola kilipofunga bao, Madrid walirudisha.

Huku Casemiro akiwa na uwezekano wa kurejea Madrid, Guardiola alisisitiza City italazimika kuwa katika ubora wao ili kutinga fainali ya Mei huko jijini Paris.

"Bila kujali matokeo, ikiwa ni 2-0 au 3-0 bado tungelazimika kwenda Bernabeu na kucheza vizuri. Tukicheza kama tulivyocheza kipindi cha pili, hatutaweza kushinda," alisema Guardiola mara baada ya mchezo huo kwenye Uwanja wa Etihad.

**"Ikiwa tutacheza kama tulivyocheza katika vipindi vingine, tutacheza. Tunataka kuwa pale ili kufanya maonyesho mazuri, hili ndilo ninalotaka kuwaambia wachezaji wangu wafanye - wasifikirie kitu kingine chochote.**

"Nilipokuwa mwanasoka na kocha, unapoenda Bernabeu lazima ufanye kama unavyojipenda au hakuna chaguo la kushinda. Lazima upitie hali hizi ili kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya."

City walikuwa hatarini vivyo hivyo katika mchezo wa pili wa robo fainali, wakishikilia uongozi wa bao moja dhidi ya Atletico Madrid kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 51 alipata faraja kutokana na ukweli City walifanikiwa kuingia kwenye nafasi hiyo, lakini akakubali wanahitaji kutambua aina hizo za fursa huko Bernabeu.

"Tulifanya kila kitu kushinda na kwa ujasiri, kwa mpira, bila mpira, hivyo tunatakiwa kuwa makini sana kwenye mchezo wa pili."

"Mpira ni mpira, matokeo ni matokeo, lakini jinsi tunavyofanya ni vya kipekee, hakuna anayeweza kusema uchezaji haukuwa mzuri, tunajua labda tunapaswa kuongeza kiwango ili tufike fainali, lakini mashindano haya yanadai hivyo."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,198

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
CHELSEA
1 | 3.02
X | 3.37
2 | 2.21

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VINICIUS AMPA BENZEMA BALLON D'OR



**MADRID,** Hispania

VINICIUS Junior amesema mchezaji mwenzake, Karim Benzema anatashili kushinda tuzo ya Ballon d'Or kwa kiwango kizuri anachokionyesha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Benzema kwa mara nyingine alikuwa kwenye kiwango kizuri kwa Real Madrid katika kichapo cha mabao 4-3 kutoka kwa Manchester City katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, akifunga bao kipindi cha kwanza na mkwaju wa penalti kipindi cha pili.

Akizungumza baada ya mchezo huo - ambapo pia alifunga bao zuri - Vinicius alisema anatumai Benzema atashinda Ballon d'Or mwaka huu.

"Hakuna maneno ambayo yanaweza kuelezea jinsi Benzema anavyocheza. Anastahili Ballon d'Or," alisema. "Natumain kaka yangu Benzema atashinda LaLiga, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ballon d'Or."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil pia alizungumzia kuhusu mchezo wenyewe, akisema hakufurahishwa na matokeo na Los Blancos wanapaswa kuimarika 'katika kila eneo' kabla ya mchezo wa pili wa wiki ijayo.

"Siwezi na sitawahi kufurahishwa na kushindwa. Tunapaswa kuimarika katika kila eneo kwa mchezo wa pili," alisema.



# Scholes asikitika United kutomtendea haki Lingar

**MACHESTER,** England

PAUL Scholes anajuta kuweka hadharani mazungumzo ya faragha na Jesse Lingard na amesema kiungo huyo "ametendewa vibaya sana" na Manchester United.

Akizungumza baada ya United kuchapwa mabao 3-1 na Arsenal Jumamosi iliyopita, Scholes alifichua Lingard alimwambia kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha Mashetani Wekundu "ni balaa" na "fujo".

Hicho kilikuwa ni kipigo cha nne mfululizo kwa United kwenye ligi ugenini, na kufanya kuwa na mbio zao mbaya zaidi tangu kupoteza mechi sita mfululizo kati ya Desemba 1980 na 1981.

Akitafakari maoni yake katika joto la sasa, Scholes amekiri hakupaswa kufichua kile Lingard alichomwambia.

Lingard alicheza dakika 13 za mwisho kwenye Uwanja wa Emirates ikiwa ni mechi yake ya 16 ya Ligi Kuu England msimu huu, ingawa ni mbili tu kati ya hizo ndizo ameanzishwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ametumika mara 22 ka mashindano yote, ju ya dakika 548 uwan - na wachezaji 19 wa cheza zaidi yake.

United inaripot kumzuia Lingard k unga na Newcastle Uni au West Ham, amb alifanikiwa kwa mk msimu uliopita, Janu na Scholes ameko jinsi klabu yake ya zam inavyomshughulikia n timu huyo wa akad yao.

"Nadhani Jesse an endewa vibaya sana klabu, kusema ukw aliongeza Scholes.

3,475,840

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/04/22 | 17:00 | Watford vs Burnley | 2.51 | 3.20 | 2.71 |
| 02. 30/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Brighton | 2.64 | 3.04 | 2.69 |
| 03. 30/04/22 | 17:00 | Southampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 04. 30/04/22 | 14:30 | Barnsley vs Preston | 2.77 | 3.27 | 2.42 |
| 05. 30/04/22 | 17:00 | Coventry vs Huddersfield | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 06. 30/04/22 | 19:00 | Sampdoria vs Genoa | 2.46 | 3.18 | 2.79 |
| 07. 30/04/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 08. 01/05/22 | 15:00 | Elche vs Osasuna | 2.99 | 3.09 | 2.42 |
| 09. 01/05/22 | 15:30 | GO Ahead Eagles vs Vitesse Arnhem | 2.59 | 3.43 | 2.49 |
| 10. 01/05/22 | 16:00 | Empoli vs Torino | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 01/05/22 | 17:15 | Granada vs Celta Vigo | 2.56 | 3.16 | 2.76 |
| 12. 01/05/22 | 19:30 | Rayo Vallecano vs Real Sociedad | 2.96 | 3.06 | 2.47 |
| 13. 01/05/22 | 21:00 | Waalwick vs Groningen | 2.68 | 3.33 | 2.46 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 28/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5455 | Jubilo Iwata vs Nagoya Grampus | 3.54 | 3.10 | 2.02 |
| 13:30 | 4783 | Pailan Arrows vs Aizawl FC | 4.27 | 3.45 | 1.74 |
| 14:00 | 4854 | Yokohama F Marinos vs Hoang Anh Gia Lai | 1.20 | 5.84 | 10.71 |
| 14:00 | 5923 | Van Yerevan vs Alashkert Martuni | 4.37 | 2.96 | 1.87 |
| 14:30 | 5893 | Kenkre FC vs Tiddim Road Athlectic Club | 4.48 | 3.45 | 1.70 |
| 15:00 | 3359 | WIT Georgia vs Metalurgi R | 2.67 | 3.20 | 2.42 |
| 15:00 | 5697 | Wigan U23 vs Swansea U23 | 1.97 | 3.51 | 3.26 |
| 16:00 | 1556 | Mbeya City vs Biashara United | 2.14 | 2.85 | 4.00 |
| 16:00 | 2886 | Malisheva vs KF Llapi | 3.00 | 3.15 | 2.38 |
| 16:00 | 3392 | KF Ballkani vs KF Drita | 1.99 | 3.26 | 3.45 |
| 17:00 | 2150 | Chiangrai Utd vs Kitchee | 1.97 | 3.21 | 3.55 |
| 17:00 | 3015 | Pdrm vs Kuching FA | 2.80 | 3.25 | 2.47 |
| 17:00 | 3879 | Selangor Pkns vs Projek Fam-Msn | 1.28 | 5.07 | 8.38 |
| 17:00 | 5521 | Sydney FC vs Jeonbuk Hyundai | 3.70 | 3.31 | 1.90 |
| 17:30 | 3885 | Real Kashmir vs Sudeva Delhi FC | 2.08 | 2.96 | 3.55 |
| 18:00 | 4079 | SK Super Nova vs FS Metta/Lu | 3.01 | 3.16 | 2.22 |
| 18:00 | 4356 | Vratimov vs Banik Ostrava B | 5.64 | 4.67 | 1.41 |
| 18:00 | 5392 | Hifk vs HJK Helsinki | 8.77 | 4.67 | 1.30 |
| 18:30 | 3166 | Urartu vs Ararat Yerevan | 1.95 | 2.97 | 3.99 |
| 18:30 | 5210 | FC KTP vs TPS Turku | 2.53 | 3.22 | 2.53 |
| 18:30 | 5874 | Arman Gohar Sirjan vs Shahrdari Astara | 2.02 | 2.77 | 4.08 |
| 19:00 | 1681 | Ida-Virumaa FC Alliance vs Paide Linnameeskond | 6.81 | 5.81 | 1.33 |
| 19:00 | 2056 | Saipa Karadj vs Shams Azar Qazvin | 1.83 | 2.82 | 5.05 |
| 19:00 | 2247 | Viljandi Tulevik vs Flora II | 10.01 | 6.61 | 1.22 |
| 19:00 | 3931 | Rayka Babol vs Pars Jonoubi Jam | 2.78 | 2.42 | 3.07 |
| 19:00 | 4033 | Esteghlal Mollasani vs Mes Shahr-e Babak | 2.48 | 2.43 | 3.50 |
| 19:00 | 4311 | Shahrdari Hamedan vs Vista Turbine | 2.37 | 2.65 | 3.65 |
| 19:00 | 4875 | OKS Odra Opole vs Puszcza Niepolomice | 2.26 | 3.07 | 3.02 |
| 19:00 | 5242 | Sandecja vs Podbeskidzie Bie | 2.67 | 3.20 | 2.42 |
| 19:00 | 5676 | Ghasghaei Shiraz vs Esteghlal Khuzestan | 3.07 | 2.53 | 2.63 |
| 19:15 | 2404 | Machine Sazi Tabriz vs Khosheh Talaei | 4.38 | 2.97 | 1.87 |
| 19:30 | 2023 | VRI vs Ringkobing IF | 3.69 | 3.89 | 1.75 |
| 19:30 | 2632 | B 1908 Amager vs Koge Nord FC | 1.86 | 3.79 | 3.36 |
| 19:30 | 4921 | Vejle BK vs Midtjylland | 5.27 | 3.61 | 1.58 |
| 20:00 | 3206 | Concordia Chiajna vs Hermanstadt | 4.28 | 3.07 | 1.85 |
| 20:00 | 3929 | Viimsi JK vs FCI Levadia Tallinn U21 | 1.69 | 4.59 | 3.85 |
| 20:30 | 2026 | Sund IF vs Ytterhogdals IK 1921 | 3.69 | 3.89 | 1.75 |
| 20:30 | 2914 | Standard Liege U21 vs KRC Genk U21 | 4.19 | 4.10 | 1.62 |
| 20:30 | 4748 | St Truiden U21 vs KAA Gent U21 | 4.38 | 4.68 | 1.52 |
| 21:00 | 4195 | Lillestrom vs Aalesunds | 1.66 | 3.93 | 4.58 |
| 21:30 | 2464 | Riffa Club vs Muharraq SC | 1.66 | 3.54 | 4.66 |
| 21:30 | 3196 | Stomil Olsztyn vs GKS Tychy | 3.26 | 3.21 | 2.07 |
| 21:45 | 1273 | Chelsea W vs Tottenham W | 1.02 | 10.68 | 38.85 |
| 21:45 | 2974 | Manchester Utd vs Chelsea | 3.02 | 3.37 | 2.21 |
| 22:00 | 1339 | Feyenoord vs Marseille | 2.15 | 3.49 | 3.14 |
| 22:00 | 1509 | Leicester vs Roma | 2.26 | 3.29 | 3.09 |
| 22:00 | 2046 | RB Leipzig vs Rangers | 1.34 | 4.91 | 8.22 |
| 22:00 | 3151 | West Ham vs Eintracht Frankfurt | 1.94 | 3.40 | 3.85 |
| 22:15 | 1586 | Vikingur Reykjavik vs Keflavik IF | 1.33 | 5.04 | 6.78 |
| 22:30 | 2649 | Zamalek vs Al Masry Club | 1.40 | 4.28 | 7.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# SIMBA SC YAWEKA WAZI HAKUNA ATAKAYEONDOKA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya nyota wake kuonyesha kiwango kizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, uongozi wa Simba umesema hakuna mchezaji atakayeondoka ambaye anahitajika katika kikosi cha hicho, imefahamika.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu alisema pia kibarua cha Kocha Mkuu, Franco Pablo bado kiko salama licha ya kuodolewa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa penalti 4-3, dhidi ya Orlando Pirates Jumapili iliyopita nchini Afrika ya Kusini.**

Mangungu ambaye alizungumzia mambo mbalimbali ya klabu hiyo, alisema Simba imepokea ofa nyingi kutoka sehemu tofauti Afrika ikitaka huduma za wachezaji wao, lakini mambo yote yatazungumzwa na kutolewa ufafanuzi baada ya msimu ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika.

"Kwa sasa klabu ya Simba ilipofikia hakuna mchezaji yoyote atakayetakiwa kubaki akaondoka, hivyo niwatoe wasiwasi wanachama na mashabiki wa Simba kuwa hakuna mchezaji yoyote tegemeo, ambaye klabu inamtaka abaki kwa msimu ujao akaondoka," alisema Mangungu.

Mwenyekiti huyo alisema wamekuwa wakiwaongeza mikataba wachezaji ambao wanatakiwa kubaki katika klabu hiyo kila muda wa kufanya hivyo unapofika na hutekeleza mchakato huo kimya kimya tofauti na timu nyingine zinavyofanya.

Kumekuwa na tetesi kuwa baadhi ya wachezaji wa Simba, akiwamo Joash Onyango huenda akajiunga na Yanga.

"Kila kitu kina wakati wake, huu ni wakati wa mashindano, bado tuna Ligi Kuu na Kombe la FA, huwezi kwa sasa kuzungumzia kocha, mara wachezaji, siyo kipindi chake. Kuhusu Pablo ni kweli hakufikia malengo tuliyompa, lakini tumefikia eneo zuri, ana mkataba wa Simba kwa sasa tumejikita kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA, hizi taarifa zinazoenezwa anaondolewa si za kweli, kwa sababu mkataba wake bado upo," alisema Mangungu.

Kiongozi huyo alisema baadhi ya wachezaji wao wanatakiwa nje ya nchi, lakini Simba imeanza kusajili wachezaji wapya akiwamo winga mchachari wa US Gendamarie, Victorien Adebayor.

"Tuna ofa na timu nyingi sana, huwezi kucheza michuano hii mikubwa, hasa kwa timu nzuri kama ya Simba halafu wachezaji wako wakakosa ofa. Kwa hiyo zipo, na hata sisi wenyewe tuna wachezaji ambao tunawafuatilia ili kuwasajili, lakini haya yote huu siyo wakati wake, niwaeleze tu wanachama na mashabiki wa Simba kuwa klabu hii ina viongozi wenye weledi mkubwa na kila kitu kitaenda sawa na watafurahi," alisema mwenyekiti huyo.

Simba imerejesha nguvu zake katika kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Kombe la FA, ambalo wanalishikilia.



Kiungo wa Azam FC, Mudathir Yahya (kulia), akiwania mpira dhidi ya Frank Domayo katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, mkoani Geita. **PICHA: MTANDAO**

# Mlandizi Queens, Ilala dimbani

**Na Saada Akida**

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu inaendelea leo kwa Mlandizi Queens kuwakaribisha Ilala Queens kwenye Uwanja wa Mabatini, mkoani Pwani.

Mechi nyingine ya ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 itawakutanisha Oysterbay Girls dhidi ya Fountain Gate Princess kutoka jijini Dodoma.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa mabingwa watetezi, Simba Queens kuwakaribisha Alliance Girls wakati TSC Queens kutoka jijini Mwanza itawafuata JKT Queens kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Mstaafu Isamuhyo.

The Tiger Queens yenyewe itakuwa nyumbani kuvaana na Yanga Princess kwenye Uwanja wa Shule ya Kimataifa ya Braeburn ya jijini Arusha.

Bingwa wa ligi hiyo ataiwakilisha Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Klabu Bingwa Afrika kwa Wanawake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Michezo
Alhamisi Aprili 28, 2022
Nipashe



Vinicius ampa Benzema Ballon d'Or UKURASA 22



Beki wa kulia wa Yanga, Djuma Shaaban ambaye anatajwa yuko katika hatihati ya kuikosa mechi dhidi ya watani wa wa jadi, Simba itakayochezwa keshokutwa kutokana na kuwa majeruhi. **PICHA: MTANDAO**

## Simba: Tutavunja mwiko

**Na Saada Akida**

HUKU ikiwa na maumivu ya kutolewa katika mashindano ya kimataifa, habari njema kwa mashabiki wa Simba ni kuhusu kurejea kwa nahodha na mshambuliaji wao, John Bocco atakayekuwa sehemu ya wachezaji watakaocheza mechi ya watani wa jadi hapo keshokutwa.

Simba watakuwa ugenini katika mechi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu alisema timu yao inaendelea vyema na maandalizi kuelekea dabi hiyo ya Kariakoo, lakini hawana mpango wa kumfuta kazi, Kocha Mkuu, Pablo Franco kufuatia timu hiyo kushindwa kufikia malengo yao ya kucheza hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika .

Mangungu alisema viongozi wa klabu hiyo wanafanya kazi kwa weledi na suala la kumfuta kazi Pablo halipo kwa sasa kama ambavyo inazungumzwa.

Alisema kocha huyo bado ana mkataba wa kukinoa kikosi cha Simba na wanahitaji kuendelea naye mpaka pale watakapofanya uamuzi mwingine tofauti.

"Hakuna taarifa yoyote iliyotolewa inayosema viongozi tutamfukuza kazi kocha kwa sababu hatukufikia malengo, Pablo bado ana mkataba na Simba ataendelea kuisuka timu yetu, klabu yetu inaendeshwa kwa weledi mkubwa hali hiyo hatuwezi kujibu kila uzushi," alisema Mangungu.

Alisema kochaa huyo anaendelea kukiimarisha kikosi chake kuelekea mchezo dhidi ya Yanga na anaamini atahakikisha wanapata matokeo ya ushindi mkubwa.

"Mashabiki waendelee kuiunga mkono timu yao kila tunapocheza, tunaenda kucheza na Yanga, tunaimani ya kushinda kwa kishindo katika mchezo huo na suala la ubingwa kila mtu kwa sasa ashinde mechi zake," alisema Mangungu.

Aliongeza mbio za ubingwa hazijafika mwisho na sasa wanaendelea kucheza mechi zao 11 zilizosalia za mzunguko wa pili.

"Kuhusu ubingwa hatujakata tamaa, ukiangalia hesabu zilivyo, Yanga wana pointi nyingi lakini sijui wana uhakika gani wa kushinda mechi zote walizobakisha mzunguko wa pili, mwanzoni mwa msimu mambo yalikuwa magumu hasa kushiriki michuano ya kimataifa pamoja na ligi ya nyumbani," alisema mwenyekiti huyo.

Aliongeza hali ya wachezaji imekuwa nzuri baada ya majeruhi wote kupona akiwamo Bocco ambaye ameanza kufanya mazoezi magumu tayari kuwakabili Yanga hapo keshokutwa.

# Yanga yaonyesha ramani ya ushindi

## ●●● Yatamba iko kamili kutia chumvi kidonda cha watani zao huku Djuma...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAKATI mabosi wa Yanga wakitamba wamejipanga vyema kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya dabi itakayochezwa keshokutwa, beki wa kulia wa timu hiyo, Djuma Shaaban, yuko katika hatihati ya kuukosa mtanange huo kutokana na kuwa majeruhi.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wachezaji wa timu hiyo wako kamili kuwavaa Simba na kila mmoja anatamani kukutana na wapinzani hao.**

Bumbuli alisema benchi la ufundi la timu hiyo linaendelea kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika mechi zilizopita na pia kukiimarisha zaidi kikosi chao kwa sababu wanahitaji matokeo ya ushindi tu na si vinginevyo.

"Timu inaendelea na mazoezi yake kwa ajili ya mchezo wetu huo tukiwa na matumaini ya kupata pointi tatu, kila mchezaji ana kiu na ari ya kuona tunapata ushindi," alisema Bumbuli.

Ofisa huyo amewaomba mashabiki wa timu hiyo wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuwashangilia wachezaji wao ambao wameahidi kupambana na hatimaye kufikia malengo.

Alisema wamejipanga kushinda mechi hiyo dhidi ya wapinzani wao ambao watakuwa wamerejea nyumbani kwa mara ya kwanza baada ya kutolewa katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Alitamba Yanga imejiandaa kikamilifu 'kutia chumvi' katika kidonda cha Simba ambayo ilitolewa katika michuano hiyo ya kimataifa kwa penalti baada ya matokeo ya jumla kuwa sare ya bao 1-1.

"Mazoezi yanakwenda vizuri, timu iko kambini Kigamboni, tuna majeruhi mmoja tu ambaye ni Djuma Shabaan aliyeumia kwenye mechi iliyopita dhidi ya Namungo, mpaka sasa yupo chini ya uangalizi wa madaktari na tutaangalia nini watasema kuhusiana na afya yake, kama majeraha yake ni makubwa, au ya kawaida tu na anaweza kucheza, " alisema Bumbuli.

Aliongeza licha ya kujipanga, wamejiandaa kukutana na upinzani kutoka kwa Simba kwa sababu hawatakubali kupoteza mchezo huo kirahisi.

"Tunawakaribisha kwenye ligi ambako kuna wafalme wake ambao ni sisi, watakuwa na kazi kubwa ya kuwatuliza mashabiki wao kwa sababu hawana kitu chochote kwa sasa. Utakuwa mchezo mzuri sana, watakuwa wamejiandaa vya kutosha kwa hiyo tunatakiwa tutoe burudani tucheze mchezo mzuri watu wafurahi. Lakini sisi tutakuwa tunacheza tukiwa na amani kwani tunaongoza kwa tofauti ya pointi nyingi, tupo kileleni na hatujapoteza, na tuko kwenye njia nzuri ya kuutwaa ubingwa, kwa hiyo hata tukipoteza mechi moja au mbili, hatuna wasiwasi sana wa kuupoteza ubingwa kutokana na pengo kubwa la pointi lililoliweka," Bumbuli alisema.

Simba mabingwa watetezi wa ligi hiyo watashuka dimbani wakiwa na mchezo mmoja pungufu wakati watani zao, Yanga wenye pointi 54 ndio vinara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >